# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR.

**RIPOTI YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**

**NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA KANUNI NA**

**SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA**

**MEZANI NA SERIKALI KWA**

**MWAKA 2023/2024.**

**February, 2024.**

# YALIYOMO

RIPOTI YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR YA MWAKA 2023/2024. .... 1

SEHEMU YA KWANZA .... 1

1.1 UTANGULIZI .... 1

1.2 MADHUMUNI YA MUHTASARI .... 6

SEHEMU YA PILI .... 13

2.0 UCHAMBUZI WA KANUNI NA MATOKEO YAKE .... 13

2.1 KANUNI ZA BENDERA NA NEMBO YA MAHAKAMA, ZANZIBAR .... 13

2.1.1 CHANGAMOTO .... 14

2.1.2 MAPENDEKEZO .... 15

2.2 KANUNI ZA WAFANYAKAZI ZA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ), 2022. .... 16

2.2.1 CHANGAMOTO .... 16

2.2.1.1 Makosa yaUandishi wa Sheria: .... 16

2.2.2 MAPENDEKEZO .... 18

2.2.3 USHAURI .... 19

2.3 KANUNI ZAWAFANYAKAZI WA SHIRIKA LA BIMA 2023 .... 19

2.3.1 CHANGAMOTO .... 20

2.3.2 MAPENDEKEZO .... 21

2.3.3 USHAURI .... 22

2.4 KANUNI ZA MASUALA YA WAZEE (UTOAJI WA HUDUMA ZA MAKAAZI) ZANZIBAR, 2023. ........ 22

2.4.1 UTANGULIZI ........ 22

2.4.2 CHANGAMOTO ........ 23

2.4.3 MAPENDEKEZO ........ 24

2.4.4 USHAURI ........ 26

2.5 AMRI YA VIWANGO VYA MWENDO VYA KITAIFA KWA BARABARA ZOTE ZA ZANZIBAR, 2023 ........ 26

2.5.1 UTANGULIZI ........ 26

2.5.2 CHANGAMOTO ........ 27

2.5.3 USHAURI ........ 27

2.5.4 MAPENDEKEZO ........ 28

2.6 KANUNI ZA THAMANI YA FIDIA ZA MAZAO NA MITI, 2023. 29

2.6.1 UTANGULIZI ........ 29

2.6.2 CHANGAMOTO ........ 29

2.6.3 MAPENDEKEZO ........ 30

2.6.4 USHAURI ........ 31

2.7 KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (FAO LA KUUMIA KAZINI) 2023. ........ 32

2.7.1 UTANGULIZI ........ 32

2.7.2 CHANGAMOTO ........ 32

2.7.3 MAPENDEKEZO ........ 33

2.7.4 USHAURI ........ 35

2.8 KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (FAO LA UPOTEVU WA AJIRA) 2022. .......... 36
2.8.1 UTANGULIZI. .......... 36
2.8.2 CHANGAMOTO .......... 36
2.8.3 MAPENDEKEZO .......... 37
2.8.4 USHAURI .......... 37
2.9 TANGAZO LA KIMA CHA CHINI CHA MISHAHARA KATIKA SEKTA BINAFSI, 2023. .......... 38
2.9.1 UTANGULIZI .......... 38
2.9.2 CHANGAMOTO .......... 38
2.9.3 MAPENDEKEZO .......... 39
2.9.4 USHAURI .......... 39
2.10 KANUNI ZA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA 2023. .......... 40
2.10.1 UTANGULIZI .......... 40
2.10.2 CHANGAMOTO .......... 40
2.10.3 MAPENDEKEZO .......... 42
2.10.4 USHAURI .......... 43
2.11 KANUNI ZA UTUMISHI ZA MAMLAKA YA UTHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR, 2013. .......... 43
2.11.1 UTANGULIZI .......... 43
2.11.2 CHANGAMOTO .......... 44
2.11.3 MAPENDEKEZO .......... 44
2.11.4 USHAURI. .......... 45

2.12 KANUNI ZA UHIFADHI NA UENDELEZAJI WA MJI MKOMGWE, 2023........................................................................ 45

2.12.1 UTANGULIZI........................................................................ 45

2.12.2 CHANGAMOTO........................................................................ 46

2.12.3 USHAURI........................................................................ 46

2.12.4 MAPENDEKEZO........................................................................ 47

2.13 KANUNI YA UDHIBITI WA HOSPITALI BINAFSI, 2023 .... 48

2.13.1 UTANGULIZI. ........................................................................ 48

2.13.2 USHAURI ........................................................................ 48

2.13.3 MAPENDEKEZO........................................................................ 50

SEHEMU YA TATU........................................................................ 51

3.1 HITIMISHO ........................................................................ 51

3.2 MWISHO........................................................................ 52

## RIPOTI YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR YA MWAKA 2023/2024.

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.1 UTANGULIZI

Naanza kwa Kumshukuru Allah (S.W) Muumba wa Mbingu na Ardhi na vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia pumzi na afya na kutuwezesha kukutana tena katika jengo hili muhimu tukiwa na dhima kubwa ya kuwawakilisha wananchi ambao wametuwezesha kuwa wawakilishi katika chombo hiki cha kutunga Sheria. Aidha Naomba kutumia fursa hii adhimu Kumshukuru Mhe, DK, Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa namna anavyoendelea kuiongoza nchi yetu kwa Hekma uadilifu na Busara ya Hali ya Juu. Maono yake ni Dira yetu katika kuwatumukia wananchi.

Vile vile, shukrani zangu nazielekeze kwako Mheshimiwa Spika na Viongozi wenzio wa Baraza kwa namna mnavyoliongoza Baraza na mnavyotoa mashirikiano ya dhati kwa Kamati yetu ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Pia siwezi kuendelea pasi na kuwashukuru wajumbe wote wa Baraza lako kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majumu yetu.

Kamati inatekeleza majukumu yake kwa mamlaka iyokasimiwa na Baraza ambalo ndio chombo cha kutunga sheria kwa mujibu wa Ibara ya 78 ya Katiba ya Zanzibar, 1984,ambayo imeipa Baraza la Wawakilishi mamlaka yote ya kutunga Sheria juu ya mambo yote ya yasiyo ya Muungano yahusuyo Zanzibar,

"*Nguvu za kutunga sheria kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano katika Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi*"

Pamoja na mamlaka hayo, Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Ibara ya 79(6) cha Katiba ya Zanzibar, 1984 limekasimu madaraka yake ya kutunga Sheria kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali kutunga sheria Ndogo ndogo *(subsidiary legislation/ delegated legislation)* ambazo hujumuisha:

Amri(Orders)

Matamko (Proclamations)

Kanuni za Taasisi (Rules)

Kanuni za Mahakama (Rules of Court)

Kanuni za Wizara (Regulations)

Tangazo

Taarifa(Notices)

Kamati inaimani kuwa kwa kiasi kikubwa Ripoti hii itawezesha Waheshimiwa Wajumbe kupata taaluma na hivyo kuweza kutoa

ushauri zaidi kuhusu Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zinazowasilishwa Barazani kupitia Kamati hii. Kabla ya kuendelea naomba nitambue ushirikiano mkubwa uliopelekea kufanikisha kazi hii ya Kamati kutoka kwa Wajumbe wa Kamati ambao wamefanya kazi kwa bidii na maarifa pasi na kuchoka. naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Mhe. Mihayo Juma Suleiman N'hunga | Mwenyekiti |
| Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | M/Mwenyekiti |
| Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | Mjumbe |
| Mhe. Hassan Hamad Omar | Mjumbe |
| Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Mjumbe |
| Mhe. Yussuf Hassan Iddi | Mjumbe |

Aidha, shughuli za Kamati hii zimekuwa zikiratibiwa na Makatibu wawili kutoka Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, ambao wametimiza wajibu wao ipasavyo katika kuhakikisha kwamba kamati yetu inatekeleza majukumu yake. Makatibu hao wamekuwa ni msaada mkubwa kwa kamati na chachu ya mafanikio ya kamati hii kwani wamekuwa wakipokea na kuchambua Kanuni zote zinazowasilishwa na kuwashauri wajumbe namna bora ya kuzifanyia kazi Kanuni hizo na kufanikisha ukamilishaji wa ripoti hii ninayoiwasilisha. Naomba nao niwataje kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Ndg. Karima Abdul- Wahab | Katibu |
| Ndg. Noman Thabit Noman | Katibu |

Vile vile, Kamati inatambua uwepo na ushiriki wa Afisa Sheria wa Wizara ya Katiba na Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Ndg. Shamail Abeid Khamis, ambaye ameshirikiana na Kamati kikamilifu katika vikao vya Kamati katika kuiwakilisha Wizara hiyo.

Sambamba na hayo napenda kumtambua Msaidizi wa Mjumbe ambaye alihakikisha kutimiza wajibu wake wakati wote ambao Kamati inafanya shughuli zake, naye ni:

| | |
|---|---|
| Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi wa Mjumbe |

Baada ya utangulizi huo naomba sasa nijielekeze katika Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa mwaka 2023/2024 baada ya shughuli mbali mbali zilizofanywa na Kamati hii katika kipindi hicho.

Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria imeendelea na kazi zake katika mizunguko yake kama ifuatavyo:

Mzinguko wa Kwanza ulikuwa tarehe **06/03/2023** hadi **24/03/2023,** Mzinguko wa Pili ulikuwa tarehe 09/10/2023 hadi 27/10/2023 Mzinguko wa Tatu ulikuwa tarehe **17/07/2023** hadi **04/08/2023 na mzunguko wa nne ulikuwa tarehe** 18**/12/2023**

hadi **5/01/2024.** Aidha Kamati hii ilipitia Sheria Ndogo Ndogo na Kanuni mbali mbali kutoka katika Taasisi tofauti kwa dhamira ya kuziimarisha ili ziweze kukidhi haja ya kuanzishwa kwake.

Kimsingi kazi ya utungaji wa Sheria ni kazi ya msingi ya Baraza la Wawakilishi. Hata hivyo Kifungu 79(6) cha Katiba ya Zanzibar, 1984, kimekasimu madaraka ya utungaji wa Sheria kwa Idara ama Maafisa wa Serikali ambapo Sheria zinazotungwa kwa utaratibu huo huitwa Kanuni ama Sheria Ndogo Ndogo.

kwa kuwa kukasimu madaraka lazima kufuatane na usimamizi (deligation and supervision) hivyo Kamati yetu ndiyo yenye jukumu la kufanya kazi ya usimamizi kwa wale waliokasimiwa madaraka hayo kwa niaba ya Baraza. Hivyo Kamati hii inapotekeleza majukumu yake inahakikisha kwamba misingi ya utungaji wa Sheria inazingatiwa na kufuatwa kikamilifu kwa kila Taasisi au Afisa Aliyekabidhiwa kazi hiyo.

Miongoni mwa mambo yanayozingatiwa katika kutunga Sheria ndogo ndogo ni pamoja na kuhakikisha Sheria inayotungwa haikiuki Misingi ya Katiba na pia mtunzi wa sheria hiyo awe amepewa Mamlaka na haendi kinyume na Sheria Mama.

Kamati yetu katika kutekeleza majukumu yake, nyezo muhimu tunazotumia kama miongozo ya kazi zetu ni kuzingatia Katiba, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sheria ya Utumishi Umma pamoja na Sheria ya Makosa ya Jinai.

Kamati hutumia njia ya kukutana na walengwa wa Kanuni (Wadau) zinazofanyiwa uchambuzi ili kufahamu hali halisi iliopo kuhusiana na Sheria husika.

Matumizi ya rejea mbali mbali zilizoandikwa na wataalamu wabobezi pia huwa ni nyezo yetu inayotusaidia kufanya mapitio ya uandishi wa Kanuni hasa suala la utaalamu na mbinu za uandishi.

## 1.2 MADHUMUNI YA RIPOTI

Ripoti hii unakusudia kueleza kwa kiasi utendaji kazi wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo, ambapo Kamati inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 107 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2020, ambayo imeainisha majukumu ya Kamati katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizo. Aidha ripoti ya Kamati imeyaainisha kiukamilifu.

Katika kutekeleza majukumu yake Kamati hutumia njia mbali mbali ili kufikia malengo.

Miongoni mwa njia hizo ni:

Kupitia nyaraka mbali mbali ambazo Kamati ilikusudia kuzifanyia kazi;

Kufanya mahojiano na maafisa wanaohusika na Kanuni hizo

Kufanya mahojiano na walengwa au watumiaji (wadau) wa Kanuni hizo na,

Kufanya ziara katika Taasisi ambazo Kanuni au Sheria Ndogo Ndogo hizo zinatumika kama kutakuwa na umuhimu wa kufanya hivyo, ili kuweza kubaini mafanikio na changamoto zao katika utekelezaji wa Kanuni hizo.

Kamati iliweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika kipindi hiki na kuweza kuchambua Kanuni zilizowasilishwa na kutoa ushauri kwa Taasisi zilizotunga nakuni hizo.

Miongoni mwa majukumu yake ni:

kufuatailia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye repoti ya Kamati ya Mwaka;

Kuchambua Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa ya masharti ya Katiba, Sheria Mama na sheria nyengine;

kujadili na kutoa mapendekezo kwa taasisi husika juu ya namna bora ya kutengeza Kanuni na sheria ndogo ndogo;

kulishauri Baraza kubatilisha Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ambazo zinakiuka masharti ya Katiba, masharti ya Sheria Mama au sheria nyenginezo za nchi;

kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kanuni za Baraza zimeweka sharti la kuwasilishwa Barazani Kanuni au Sheria ndogondogo iliyotungwa na Mamlaka nyingine nje ya Baraza la Wawakilishi baada ya kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. Aidha, Kanuni zimetoa fursa kwa Kamati

kuitisha Kanuni yoyote kwa lengo la kuipitia. Baada ya Baraza la Wawakilishi kupokea Kanuni hizo, Kamati hufanya uchambuzi wake na baadae kutoa maoni na ushauri ya Kanuni husika.

Kamati katika kutekeleza majukumu yake imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kufikia malengo. Mbali na mafanikio tuliyoyapata pia kuna changamoto zilizojitokeza.

Changamoto kubwa inayoendelea ni kuwa bado baadhi ya Kanuni zilizowasilishwa zimeandikwa kwa lugha ya kiengereza jambo ambalo lilifanya Kamati ishindwe kuzifanyia mapitio Kanuni hizo hasa ukizingatia kuwa nyaraka zinazowasilishwa Barazani ikiwemo Kanuni zinahitaji kuandikwa kwa lugha ya kiswahili kwani ndio lugha rasmi ya Baraza (Rejea: *Kanuni ya 25 ya Kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2020)*. Kutokana na changamoto hiyo Kamati inasisitiza kwamba Kanuni hizo ziwasilishwe tena zikiwa katika lugha ya Kiswahili.

Jumla ya Kanuni ishirini (20) zilizowasilishwa ambazo kumi na nne (14) kati ya hizo ni Kanuni za kiswahili na sita ni za Kingereza ambazo ni:

KANUNI ZA UTUMISHI ZA MAMLAKA YA UTHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR, 2023.

KANUNI ZA MASUALA YA WAZEE (UTOAJI WA HUDUMA ZA MAKAAZI) ZANZIBAR, 2023.

KANUNI ZA WAFANYAKAZI ZA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ), 2022.

KANUNI ZA WAFANYAKAZI WA SHIRIKA LA BIMA, 2023.

KANUNI ZA BENDERA NA NEMBO YA MAHAKAMA, ZANZIBAR, 2023.

KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (FAO LA KUUMIA KAZINI) 2023.

AMRI YA VIWANGO VYA MWENDO VYA KITAIFA KWA BARABARA ZOTE ZA ZANZIBAR, 2023.

KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (FAO LA UPOTEVU WA AJIRA) 2022.

KANUNI ZA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA 2023.

KANUNI ZA THAMANI YA FIDIA ZA MAZAO NA MITI, 2023.

KANUNI ZA UHIFADHI NA UENDELEZAJI WA MJI MKOMGWE, 2023.

KANUNI ZA UDHIBITI WA HOSPITAL BINAFSI, 2023.

TANGAZO LA KIMA CHA CHINI CHA MISHAHARA KATIKA SEKTA BINAFSI, 2023.

KANUNI ZA MAAKAZI YA WATOTO YALIYOKUBALIWA, 2017.

THE ANTI-MONEY LAUNDRY AND PROCEEDS OF CRIME (AMENDMENT) REGULATIONS, 2023 MADE UNDER SECTION 87 OF THE ANTI-MONEY LAUNDRY AND PROCEEDS OF CRIME ACT, NO.10 OF 2009.

ORDER FOR AMENDMENT OF FIRST SCHEDULE MADE UNDER SECTION 4(2) THE EXCISE DUTY ACT, NO.8 OF 2017.

THE WEIGHTS AND MEASURES GENERAL REGULATIONS 2023 MADE UNDER SECTION 57 OF THE WEIGHTS AND MEASURES AGENCY ACT NO.6 OF 2020.

THE ZANZIBAR BROADCASTING LICENSING (AMENDMENT) REGULATIONS, 2023 MADE UNDER SECTION 29(1) OF THE ZANZIBAR BROADCASTING COMMISSION ACT, NO. 7 OF 1997.

THE BORROWING, LENDING, GRANDS AND DEBT MANAGEMENT REGULATIONS, 2021 MADE UNDER 40,70 AND 82 OF THE PUBLIC FINANCE MANAGEMENT ACT, NO.12 OF 2012.

DECLARATION OF THE COMPULSORY STANDARDS AND NATIONAL STANDARDS MADE UNDER SECTION 16 (2) AND 17 OF THE ZANZIBAR STANDARD ACT NO. OF 2011.

Katika kuzifanyia mapitio Kanuni hizo Kamati ilitaka kujiridhisha juu ya hoja zifuatazo:

Utaratibu mzima uliotumiwa na Wizara au Taasisi katika kutunga Kanuni husika.

Sababu zilizopelekea kutungwa kwa Kanuni hiyo.

Ushirikishwaji wa Wataalamu mbali mbali wa Ndani na Nje ya Taasisi.

Ushirikishwaji wa Wadau wanaohusika na Kanuni hizo.

Baadhi ya Kanuni, Sheria zake ni za muda mrefu Kamati ilitaka kufahamu kwa nini zilichelewa kutungwa.

Changamoto zilizojitokeza kabla ya kutungwa Kanuni hizo katika utekelezaji wa Sheria.

Kulikuwa na utaratibu gani uliotumika kabla ya kutungwa kwa Kanuni hizi na ulikuwa na mapungufu gani pamoja na hayo Kanuni hizi zitaweza kuondoa kasoro hizo.

Kamati wakati wa uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zilizowekwa Mezani. Mambo yafuatayo huwa yanazingatia:

Iwapo Kanuni na Sheria Ndogo ndogo husika inakiuka Katiba ya Zanzibar, 1984;

Iwapo Kanuni na Sheria Ndogo ndogo husika inavuka mipaka au kwenda kinyume na masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutunga Kanuni na Sheria Ndogo hizo au Sheria nyingine yoyote;

Iwapo Kanuni au Sheria Ndogo Ndogo husika imezingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria *(drafting principles)*;

Iwapo Kanuni au Sheria Ndogo Ndogo husika inakiuka misingi ya haki za binadamu;

Iwapo Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo inatekelezeka kwa urahisi kiuchumi na kijamii; na

Makosa ya uandishi na uchapaji.

Kamati katika kutekeleza wa majukumu yake ilibaini mambo kadhaa kama vile Makosa ya Kimuundo, Makosa ya kuandishi, Kimaana, Kiuchapaji na Kisarufi.

Kamati ilizingatia kasoro ilizozibaini na kupendekeza marekebisho na hatua za kuchukua. Miongoni mwa kasoro zilizobainika ni;

Baadhi ya Kanuni zilizowasilishwa katika Kamati hazikuwa zimetangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. Kinyume na utaratibu wa uandishi wa Kanuni.

Baadhi ya Kanuni zimeandikwa bila ya kuzingatia vifungu wezeshi (enable provision) vya Sheria husika.

Baadhi ya Kanuni zimeonesha kugongana na Kanuni nyengine au Sheria.

Baadhi ya Kanuni zimeonesha makosa bila ya kuonesha adhabu inayotokana na kosa hilo.

Baadhi ya Kanuni hazikuonesha uhalisia wa utekelezaji wa amri inayotolewa na Kanuni hiyo.

Baadhi ya Kanuni hazikufuata utaratibu au mfumo wa uandishi wa Sheria.

Hayo yote ni makosa katika uandishi wa Sheria na Kanuni.

Kamati kabla ya kufanya uchambuzi wa Kanuni au Sheria Ndogo Ndogo hulazimika kuipitia Sheria iliyotoa Kanuni hiyo pamoja na

Kanuni husika ili kupata uwelewa na kuweza kufanya uchambuzi utakaosaidia kuimarisha Kanuni hizo.

utaratibu wa kupitia Kanuni na Sheria ndogo ndogo, Kamati huangalia kwa kina maeneo yote ya Sheria yanayopaswa kutungiwa Kanuni na kuangalia kuwa Kanuni hizo zimeenda sambamba na matakwa ya Sheria na kuakisi hali iliyokusudiwa.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UCHAMBUZI WA KANUNI NA MATOKEO YAKE

### 2.1 KANUNI ZA BENDERA NA NEMBO YA MAHAKAMA, ZANZIBAR

Kanuni hii inatokana na Sheria ya Utawala wa Mahakama, Namba 11 Mwaka 2018, Kanuni yake ni ya mwaka 2023, ambapo Jaji Mkuu amepewa uwezo chini ya kifungu 50(1) kutunga Kanuni hizi. katika kujiridhisha iwapo utaratibu wa kawaida wa utungaji wa Kanuni wa ushirikishwaji wa Wadau umefuatwa ndani ya Kanuni hizi. Kamati, ilifanya mahojiano na Taasisi husika, ili kujiridhisha kwamba Wadau walipatiwa fursa ya kushiriki katika utungwaji wa Kanuni hizo.

Kamati ilibaini kwamba, ushirikishwaji wa Wadau kwa kiasi kikubwa ulifanyika, hata hivyo; ushikishwaji huo kwa upande wa Unguja tu. Kamati inashauri ni vyema ushirikishwaji wa Wadau uwe kwa Unguja na Pemba. Hivyo Taasisi wakati wa kutunga Kanuni wanapaswa kuhakikisha ushirikishwaji wa Wadau uwe

umezingatiwa kwa eneo kubwa zaidi ili kuepusha changamoto zinaweza kujitokeza.

### 2.1.1 CHANGAMOTO

Katika kuzifanyia uchambuzi Kanuni hizi, Kamati imeona kwa ujumla Kanuni imeweza kuandikwa vizuri kwani zimefuata utaratibu wa uandishi, hata hivyo kuna baadhi ya changamoto chache zimejitokeza za makosa ya uandishi wa Sheria, miongoni mwa hizo ni:

#### 2.1.1.1 Makosa ya uandishi wa Sheria:

a) Kanuni haikuweka Kanuni za adhabu kwa mtu anayekiuka masharti yaliyowekwa na Kanuni.

b) Kanuni ya 5, imeweka mazingira ambayo Jaji Mkuu anaweza kupeperusha bendera, hata hivyo Kanuni hiyo imekosa kuainisha kuwa Jaji Mkuu anaweza kupeperusha bendera katika gari yake, wakati kiongozi huyo kwa kawaida hupeperusha bendera.

c) Kanuni haijaweka utaratibu wa kuteketeza bendera pindi ikiwa imechakaa wala haiwezi kutumika tena kwani kwa kawaida suala hilo huoneshwa katika Kanuni au sheria.

#### 2.1.1.2 Makosa ya Kimantiki:

Kanuni imeshindwa kuonesha kipimo cha rangi na ukubwa wa bendera na nembo kwani kawaida rangi za bendera na ukubwa wa nembo huainishwa katika Kanuni au sheria, Kanuni hizi hazijazingatia hayo.

Kukosekana kwa hilo tunaweza kupata Bendera au Nembo zenye Rangi zisizofanana hasa zinapotengenezwa na Viwanda Tofauti.

#### 2.1.1.3 Makosa ya Uandishi.

Kamati imebaini makosa ya kiuandishi na uchapaji ambayo yakibaki kama yalivyo yanaweza kulete athari kubwa kwa Kanuni hizi. Makosa ya aina hiyo yanaweza kubadili maana iliyokusudiwa au kuleta utata na kupelekea dhamira ya Kanuni hizo kushindwa kufikiwa.

Kamati iliweza kuyaona na kuyazingatia pamoja na kuyafanyia marekebisho makosa hayo ambayo yameainishwa katika Kiambatanisho Namba 1 cha Ripoti hii.

### 2.1.2 MAPENDEKEZO

Kamati inapendekeza Mamlaka husika kuhakikisha inafanyia kazi marekebisho yote yalioainishwa na Kamati katika kiambatanisho hicho.

## 2.2 KANUNI ZA WAFANYAKAZI ZA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ), 2022.

Kanuni hizi inatokana na kifungu cha 12 cha Katiba ya Benki ya Watu wa Zanzibar. Kanuni yake ni ya mwaka 2022, ambapo Bodi imepewa uwezo wa kisheria kutunga Kanuni hizo.

Katika kujiridhisha iwapo utaratibu wa kawaida wa utungaji wa Kanuni na ushirikishwaji wa Wadau umefuatwa wakati wa kutungwa kwa Kanuni hii. Kamati, ilifanya mahojiano na Taasisi husika ili kujiridhisha kwamba Wadau walipatiwa fursa ya kushiriki katika utungwaji wa Kanuni. Aidha, Kamati ilibaini kwamba, ushirikishwaji wa Wadau kwa kiasi kikubwa ulizingatiwa kwani wadau waliweza kuonesha maoni yao yaliozingtiwa ndani ya Kanuni hizo.

### 2.2.1 CHANGAMOTO

Katika kuifanyia uchambuzi Kanuni hii, Kamati imeona kwa ujumla Kanuni haikuzingatia matakwa ya uandishi wa kisheria, miongoni mwa changamoto kubwa zilizogundulika katika Kanuni hizo ni:

#### 2.2.1.1 Makosa yaUandishi wa Sheria:

**a)** Kanuni husika iliyowasilishwa katika Kamati haionekani kama ilitangazwa katika ***Gazeti Rasmi la Serikali jambo ambalo ni sharti la lazima kwa kuzingatia masharti***

***ya kifungu cha 36 na 37 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, nambari 7/1984.***

**b)** Kanuni ya **"kuondolewa na kubakiza**" **(Revoke and Replace)** kiutaratibu wa kiuandishi huonekana mwisho wa Kanuni husika lakini ndani ya Kanuni hizi, Kanuni hii imejitokeza ndani ya Kanuni za mwanzo za sehemu ya kwanza (**masharti ya awali)** ambapo ipo katika Sehemu ya Kwanza (1.1) kwa kawaida hukaa katika Kanuni za mwisho (masharti mengineyo) na yalipaswa kusomeka kama ifuatavyo:

"***Kanuni za wafanyakazi za mwaka 2001, zinaondolewa.***

***b) Bila ya kuathiri kuondolewa kwa Kanuni hizo jambo lolote halali lililofanywa au lililoachwa kufanywa na Kanuni zilizoondolewa litazingatiwa kuwa kimefanywa na Kanuni hizi."***

**c)** Kanuni hizi sehemu hii (1.1) haijaonesha mambo hayo tu ya msingi, bali imesheheni maelezo ambayo mengine hayapaswi kuwepo katika sehemu hiyo.

**d)** Kanuni imetumia Vichwa vya Habari (**Head note)** badala ya maneno ya pembeni (**Maginal note)** ieleweke kwamba kila nchi inao utaratibu wa uandishi wake wa Sheria (indoor policy) ambayo hulazimika kufuatwa, utaratibu wetu wa ndani upo tofauti ilivyoandikwa Kanuni hizi.

e) Kanuni imekosa kuonesha mpangilio wa sehemu kwa mujibu wa utaratibu wa matakwa ya Uandishi wa Sheria. Aidha, katika uandishi wa kisheria kila sehemu huwa na maana yake na maudhui husika.

Kamati iliweza kuyaona na kuyazingatia pamoja na kuyafanyia marekebisho makosa hayo ambayo yameainishwa katika Kiambatanisho Namba 2 cha Ripoti hii**.**

### 2.2.2 MAPENDEKEZO

Kamati inapendekeza yafuatayo:

**i.** Benki ya Watu wa Zanzibar wawasilishe mbele ya Kamati, Kanuni iliyotangazwa kisheria badala ya Rasimu ya Kanuni.

**ii.** Benki ya Watu wa Zanzibar kuangalia upya jina refu la Kanuni na iwekewe kifungu kinachoipa Mamlaka (uwezo) Bodi kuanzisha Kanuni hizi. (Enable Provision).

**iii.** Kanuni hizi itakapowasilishwa iwasilishe Pamoja na Katiba ya Benki ili kujiridhisha iwapo imezingatiwa Kikamilifu.

**iv.** Benki ya Watu wa Zanzibar, itakapowasilisha Kanuni hizi ifuate utaratibu wa uandishi wa Sheria ambapo rasimu iliyowasilishwa ilikosa kufuata **Mfumo wa Uandishi wa Kanuni na badala yake** Kanuni hizo inaonekana ipo zaidi katika simulizi au maelezo (narration).

Aidha, Mapendekezo mengine yatakuwepo katika Kiambatanisho Nambari 2 cha Ripoti Hii.

### 2.2.3 USHAURI

Kamati inashauri Benki ya Watu wa Zanzibar kuzingatia utaratibu wauandishi wa kisheria ili iweze kukidhi matakwa ya uandishi kwa mujibu wa Sheria ya Tafrisi ya Sheria. Aidha, suala la kuitangaza katika ***Gazeti Rasmi la Serikali jambo ambalo ni sharti la lazima kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 36 na 37 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, nambari 7/1984.***

Aidha, kwa kuwa Kanuni hizi ilikuwa haina miguu ya kusimamia mbele ya mahkama na kuwa imebeba haki za watu hivyo ni vyema ikafanyiwa marekekbisho hayo haraka ili iweze kusimama kisheria.

## 2.3 KANUNI ZAWAFANYAKAZI WA SHIRIKA LA BIMA 2023

Kanuni hizi zinatokana na kifungu cha 26(1) cha Sheria ya Msajili wa Hazina Namba 6 ya Mwaka 2021, ambapo Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Bima Zanzibar imepewa uwezo wa kisheria kutunga Kanuni hizo.

katika kujiridhisha iwapo utaratibu wa kawaida wa utungaji wa Kanuni na ushirikishwaji wa wadau umefuatwa ndani ya Kanuni hizi. Kamati, ilifanya mahojiano na Taasisi husika ili kujiridhisha kwamba Wadau walipatiwa fursa ya kushiriki katika utungwaji wa Kanuni hizo. Kamati ilibaini kwamba, ushirikishwaji wa wadau

kwa kiasi kikubwa ulizingatiwa kwani wadau waliweza kuonesha maoni yao yaliozingtiwa ndani ya Kanuni hizo.

### 2.3.1 CHANGAMOTO

Katika kuifanyia uchambuzi Kanuni hii, kamati imeona kwa ujumla Kanuni haikuzingatia matakwa ya uandishi wa kisheria, miongoni mwa changamoto kubwa zilizogundulika katika Kanuni hiyo ni;

1. Makosa ya Uandishi wa Kisheria
   a) Kamati imebaini kuwa Kanuni husika zilizowasilishwa haikutangazwa katika ***Gazeti Rasmi la Serikali jambo ambalo ni sharti la lazima kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 36 na 37 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, nambari 7/1984.***
   b) Kamati imebaini kuwa Kanuni hizo iliyowasilishwa hazikuonesha kifungu kinachota mamlaka ya kutungwa kwa Kanuni hizo.

   c) Kamati imebaini Kanuni ilizowasilishwa zilikosa kufuata utaratibu wa uandishi wa kisheria kama vile sehemu ya kwanza kikawaida ya uandishi huwa inaanza na **Masharti ya Awali** ambapo mara nyingi huwa na vifungu au Kanuni mbili hadi tatu. Kanuni hii imeanza na "**Utangulizi"** badala ya maneno **"Masharti ya Awali".**
   d) Kamati imebaini Kanuni ya 1 kuwepo na changamoto ya uandishi wa maneno ya pembeni yanasomeka **"Jina**

**tarehe na kuanza kutumika"** ambapo kiuandishi wa kisheria unahitaji kuandikwa maneno hayo ya pembeni **"jina na fupi na kuanza kutumika"** ambao huo ndio uandishi sahihi wa kisheria.

Kamati iliweza kuyabaini na kuyazingatia pamoja na kuyafanyia marekebisho mapungufu hayo ambayo yameainishwa katika Kiambatanisho Namba 3 cha Ripoti Hii.

### 2.3.2 MAPENDEKEZO

Kamati inapendekeza yafuatayo:

1. Shirika la Bima la Zanzibar kuhakikisha kuwa wanaweka kifungu sahihi kinachowapa uwezo wa kutungwa Kanuni husika na aliyepewa Mamlaka hayo kisheria.

2. Sehemu ya kwanza kufutwa maneno **"Utangulizi"** na badala yake kuandika upya maneno **"Masharti ya Awali"**.

3. Kanuni ya 1 kuweka maneno ya pembeni yanayosomeka kama ifuatavyo:

   **"Jina fupi na kuanza kutumika"** badala ya maneno **"jina na tarehe kuanza kutumika".** Kwenye Kanuni hii inatakiwa ionekane jina refu la Kanuni, Kanuni itaanza kutumika muda gani, baada ya kutiwa Saini na nani na kama itatangazwa kwenye gazeti basi litajwe Gazeti Rami la Serikali. ***Kama inavyoshurutishwa katika kifungu cha 36 na 37 cha Sheria ya Ufafanuzi Nam.7 ya 1984.***

4. Aidha, Mapendekezo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 3 ndani ya Ripoti hii, hivyo kamati inasisitiza kuzingatiwa mapendekezo hayo ipasavyo.

### 2.3.3 USHAURI

Kamati inashauri Kanuni za wafanyakazi wa Shirika la BIMA kuzingatia utaratibu wauandishi wa kisheria ili Kanuni iweze kukidhi matakwa ya uandishi kwa mujibu wa Sheria. Kimsingi Kanuni zinaweza kutungwa endapo ndani ya Sheria wezeshi kuwepo kifungu ambacho kitatoa Mamlaka ya utungwaji wa Kanuni husika, hivyo Kamati inashauri Shirika hilo kuhakikisha mazingatio hayo yanafuatwa kikamilifu. Aidha, kwa kuwa Kanuni hii ilikuwa haina miguu kusimama mbele ya mahakama na kuwa imebeba haki wa watu hivyo ni vyema ikafuata utaratibu ili iweze kusimama kisheria.

## 2.4 KANUNI ZA MASUALA YA WAZEE (UTOAJI WA HUDUMA ZA MAKAAZI) ZANZIBAR, 2023.

### 2.4.1 UTANGULIZI

Kanuni hizi zinatokana na kifungu cha 37 cha Sheria ya Masuala ya Wazee, Namba 2 ya mwaka 2020, ambapo Waziri amepewa uwezo wa kisheria kutunga Kanuni hizo.

Katika kujiridhisha iwapo utaratibu wa kawaida wa utungaji wa Kanuni na ushirikishwaji wa Wadau umefuatwa ndani ya Kanuni hizi. Kamati, ilifanya mahojiano na Taasisi husika ili kujiridhisha kwamba Wadau walipatiwa fursa ya kushiriki katika utungwaji wa Kanuni hizo. Aidha, kamati ilibaini kwamba, ushirikishwaji wa wadau kwa kiasi kikubwa ulizingatiwa kwani Wadau waliweza kuonesha maoni yao yaliozingatiwa ndani ya Kanuni hizo.

Hata hivyo, baadhi ya maoni yao hayakuzingatiwa kikamilifu ambayo yamejitokeza kama changamoto kubwa ndani ya Kanuni hizo. Mfano wa hayo niumri wa mzee ambapo kwa mujibu wa Shirika la kazi duniani (ILO) imeweka kiwango cha umri wa uzee ni miaka sitini, lakini Kanuni hizi imeweka umri wa miaka 70 kwa mujibu wa Sheria ya Masuala ya Wazee nambari 2 ya mwaka 2020 ndio umri wa mzee. Ambao maoni hayo waliyawasilisha kama ni miongoni mwa mambo ya kuzingatiwa.

### 2.4.2 CHANGAMOTO

Katika kuifanyia uchambuzi Kanuni hizi, Kamati imeona kwa ujumla Kanuni imezingatia matakwa ya uandishi wa kisheria, miongoni mwa changamoto kubwa zilizogundulika katika Kanuni hiyo ni:

a) **Makosa ya Uandishi wa Kisheria.**
   Baadhi ya maneno yametumika sana katika Kanuni na bila kuwekwa katika ufafanuzi.

### 2.4.3 MAPENDEKEZO

Kamati baada ya kupitia Kanuni hiyo inapendekeza yafuatayo;

1. Kanuni ya 4(5) inarekebishwa kwa kuongeza Maneno yafuatayo mwishoni mwa Kanuni hiyo:

   "**Endapo zitapita siku kumi na nne bila ya ombi la muombaji kujibiwa au kupewa taarifa yoyote iiliyorasmi itachukuliwa kuwa maombi hayo yamekubaliwa".**

2. Kuandikwa Kanuni mpya ya 7 ambayo itazungumzia mambo yafuatayo:
   1. **waziri atashughulikia rufaa ndani ya siku kumi na nne tokea tarehe ya kuwasilishwa rufaa hiyo,**
   2. **katika kushughulikia rufaa waziri anaweza;**
      - i. **kukubaliana na maamuzi ya Mkurugenzi au kukataa pamoja na kuainisha sababu,**
      - ii. **kutoa maelekezo kwa Mkurugenzi au**
      - iii. **kumtaka Mkurugenzi alizingatie tena ombi husika.**

3. Kanuni ya 7 kuwa Kanuni ya 8 na Kanuni zinazofuata zifuate mpangilio wake.
4. Kanuni ya 7 ambayo kwa sasa itakuwa Kanuni ya 8 inarekebishwa kama ifuatavyo;

- Aya ya (a) kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo” **“jina la muombaji anayeanzisha makaazi”.**
- Aya ya (f) Mkurugenzi anatakiwa aziweke wazi Taarifa zote zinazotakiwa ndani ya Kanuni hizi. Aidha, Kamati inapendekeza kuongezwa maneno **“kwa maslahi bora ya wazee”** mwishoni mwa aya hiyo.

5. Kanuni ya 8, Kamati inapendekeza katika wajumbe wa Kamati ya Tathmini Mkurugenzi atoke kwa sababu Kamati hiyo ikimaliza kazi yake Ripoti inawasilishwa kwake.
6. Kanuni ya 7(3) Kamati inapendekeza kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

7(3) (a) **“daftari la kumbukumbu la usajili litakuwa chini ya usimamizi wa Mkurugenzi**”.

(b) “**Mkurugenzi anaweza kukasimu madaraka ya usimamizi wa daftari la kumbukumbu kwa Afisa wa Ustawi wa Jamii yeyote anayeona anafaa.”**

7. Sehemu ya Pili ya Kanuni, Kamati inapendekeza kufutwa kwa Kichwa cha Habari **“TARATIBU ZA USAJILI**” na kuwekwa badala yake **“KUANZISHWA KWA MAKAAZI”.**

Kamati iliweza kuyaona, kuyazingatia na kupendekeza kufanyiwa marekebisho makosa hayo na mengine ambayo yameainishwa katika Kiambatanisho Namba 4 cha Ripoti hii.

### 2.4.4 USHAURI.

1. Kamati inashauri kuongeza maneno yafuatayo katika ufafanuzi:

a) **"Muombaji"**

b) **"Taasisi"**

c) Kanuni imekosa kuweka bayana utaratibu wa kushughulikia Rufaa.

d) Kamati inashauri tafsiri ya neno **"Mzee"** lizingatiwe kwa kuangalia Sheria nyingine na Miongozo ya Kimataifa.

e) Kamati inashauri Wizara husika kuzifanyia kazi Kanuni za wazee kwa kuzingatia marekebisho yaliyoainishwa katika kiambatanisho Namba 4 ili Kwenda sambamba na uhalisia wa uwandishi wa kisheria.

## 2.5 AMRI YA VIWANGO VYA MWENDO VYA KITAIFA KWA BARABARA ZOTE ZA ZANZIBAR, 2023.

### 2.5.1 UTANGULIZI

Kanuni hizi zinatokana na Sheria Nambari 7/2003. Chini ya kifungu 144(1) Kamati imepitia na kujirisha kuwa utaratibu wa kutungwa Kanuni/Amri hii umefuatwa.

Hata hivyo; baada ya kupitia Amri hii kwa kina pamoja na kukutana na Wadau ilibaini kasoro na changamoto kadhaa. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:

### 2.5.2 CHANGAMOTO

1. Kukosekana kwa uelewa kwa baadhi ya Wadau juu ya uwepo wa Amri ya viwango vya mwendo vya Kitaifa kwa Barabara zote.
2. Kukosekana kwa ufafanuzi wa baadhi ya maneno ambayo ni muhimu kuwepo ndani ya Amri hiyo.
3. Aidha, suala la kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari juu ya uwepo wa Amri hiyo ya viwango vya juu vya mwendo kwa maeneo ya mjini na vijiji halijafanyika kikamilifu.
4. Suala la vyombo (**vya chaji**) ambavyo havisajiliwi utaratibu wake uwekwe wazi katika Amri hiyo.

### 2.5.3 USHAURI

Mbali na hayo Kamati ilibaini kasoro na kushauri mapendekezo yafuatayo:

1. Katika Amri ya 2, ya ufafanuzi wa neno **"dereva"** Kamati inashauri kufanyiwa marekebisho katika aya ya (b) kwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

   **"Kuhusiana na gari inayovutwa inamaanisha mtu anayeendesha gari inayovuta".**

2. Kamati inashauri kuwekwa tafsiri ya maneno;

**"Kumaliza kosa, maeneo ya biashara, maeneo hatarishi, vivuko na sehemu za huduma za jamii"** kwa mujibu wa Amri hii.

3. Kamati inashauri Amri hizo ziwekewe Amri inayoonesha mawanda ya matumizi ya Amri hizo na kusomeka kama ifuatavyo:

**"Amri hizi zitatumika kwa vyombo vyote vya moto vinavyoendeshwa katika barabara zote za Zanzibar"**

4. Amri ya 3(1) inarekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo;

**"Kutakuwa na kiwango cha juu cha mwendo barabara zote katika maeneo ya mjini na vijijini kama ilivyoelezewa katika jadweli la kwaza la Amri hizi."**

### 2.5.4 MAPENDEKEZO

Kamati inapendekeza kama ifuatavyo:

1. Wizara husika kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na viwango vya mwendo vya barabarani
2. Kupatiwa kwa vitendea kazi kwa maafisa usalama barabarani ili kuwekwa kutekelezeka amri hizi.
3. kuhakikisha Alama za Barabarani kuwekwa katika barabara zote zinazohitajika ili kwenda sambasamba na Amri husika.
4. Kuangaliwa upya utaratibu uliowekwa kwa gari za kubebea wageni (private hire) kwani Amri hizi haijatambua upekee wake na ndizo zinaongoza matatizo katika barabarani.
5. Mamlaka husika kusimamia suala la kuviondoa na kuvichukulia hatua baadhi ya vyombo ambavyo

vinaendeshwa vikiwa na vimurimuri kinyume na Sheria. Sambambamba na kuviekea miongozo baadhi ya vyombo vilivyokubalikwa kufungwa vimurimuri, ili kuhakikisha Amri hii inasimamiwa ipasavyo na kuepusha migongano ndani ya barabara.

Aidha, mapendekeza mengine yameoneshwa katika Kiambatanisho Namba 5 cha Ripoti.

## 2.6 KANUNI ZA THAMANI YA FIDIA ZA MAZAO NA MITI, 2023.

### 2.6.1 UTANGULIZI

Kanuni hizi inatokana na Sheria Namba 5 ya 2015. Chini ya kifungu cha 39(1).

Kamati baada ya kupitia Kanuni za Thamani ya Fidia za Mazao na Miti pamoja na kukutana na Wadau ilibaini kasoro na changamoto kadhaa. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:

### 2.6.2 CHANGAMOTO

1. Wadau waliohudhuria kikao wengi wao sio ambao walishiriki katika utungwaji wa Kanuni hizi. Jambo ambalo linasababisha kukosekana kwa muunganiko wa taarifa.

2. Kukosekana kwa ufafanuzi wa baadhi ya maneno ambayo ni muhimu kuwepo ndani ya Kanuni hii.
   Mfano neno “**eka, ekari, shina, koongo na tuta**”.

3. Kutumika maneno mawili tofauti yakiwa na maana moja. Hili ni kosa katika uandishi. Mfano, neno “**eka na ekari**” yametumika yakiwa na maana moja.

4. Kamati imebaini pia Kanuni imekosa kuwa na Kanuni inayoonesha Mawanda ya matumizi ya Kanuni.

### 2.6.3 MAPENDEKEZO

Mbali na Changamoto hizo Kamati inapendekeza Kufanyiwa Marekebisho Kanuni hiyo kama ifuatavyo.

1. kuwekwa Mawanda ya Kanuni hizo (scope) inayoonesha mawanda yake.

2. Kanuni ya 3 inarekebishwe kwa kufuta neno **“zinafutwa”** na kuweka **“zinaondolewa” (revoked)** kwani neno kufutwa ni utaratibu wa ufutaji wa Sheria Mama (Repealed) kama inavyolekeza katika ***Sheria ya Tafsiri ya Sheria Namba 7 ya 1984, chini ya kifungu cha 28***.

3. Kuangaliwa tena Zao la Miwa liliomo ndani ya jadweli, kuthaminishwa kwa **“tuta”** ambapo haioneshi uhalisia wake.

4. Kuangaliwe upya kwa bei za baadhi ya mazao kulingana na hali halisi ya soko na gharama za kuandaa shamba mpaka kupatikana kwa mazao hayo miongoni mwa mazao ambayo ilishauriwa kuangaliwa upya thamani za fidia kama

yafuatayo; **fiwi, vanilla, hiliki, mbatata, miti kama mianzi na mengineyo**.

5. Kuangalia upya bei ya aina ya migomba baina ya mtwike na jamii ya mzuzu.

6. Kupatiwa ufafanuzi katika jadweli kwamba kuna baadhi ya mazao yanaonekana yameekewa daraja zao lakini kuna nyengine hayakuwekewa.

Aidha, mapendekezo mengine yameoneshwa katika Kiambatanisho Namba 6 cha Ripoti.

### 2.6.4 USHAURI

1. Kamati inashauri kuwekwa kwa ufafanuzi wa maneno ambayo yatasaidia kuifanya Kanuni hizi kunasomeka vizuri zaidi na kuweza kufahamika kwa urahisi.
2. Kamati, inashauri kuwa madhumuni ya Kanuni hizi yaende sambamba na yaliomo ndani ya Kanuni inayokusudia kulipa Fidia za Miti na Mazao kwa kawaida kinachopewa thamani ni mti na sio tunda linalotokana na mti kwani kamati imebaini baadhi ya vichwa vya habari vinazungumzia matunda badala ya miti mfano;
   **a. mazao jamii ya ndimu ilipaswa kuwa miti ya jamii ya ndimu,**
   **b. matunda ilipaswa kuwa ni miti ya matunda, n.k.**

3. Kamati inashauri utaratibu wa ulipaji wa fidia usiwe unachukuwa muda mrefu baada ya kufanywa kwa tathmini. Aidha, Miongozo ya ulipaji wa fidia iandaliwe ili iweze kutumika na kurahisisha uwelewa kwa masuala ya fidia kwa wahusika.
4. Kamati inashauri suala la fidia ya haki ya ardhi nalo lizingatiwe.

## 2.7 KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (FAO LA KUUMIA KAZINI) 2023.

### 2.7.1 UTANGULIZI

Kanuni hizi zimetungwa chini ya Sheria Namba 2 ya 2005, chini ya Kifungu cha 44(1).

Kamati imepata fursa ya kupitia Kanuni hizi Pamoja na kukutana na Wadau kwa lengo la kuimarisha Kanuni hizi na kuhakikisha kuwa iwapo utaratibu wa uandishi wa Sheria umefuatwa kikamilifu.

### 2.7.2 CHANGAMOTO

Kamati ilibaini changamoto kadhaa wakati wa upitiaji wa Kanuni hizi. Miongozi mwa changamoto hizo ni:

1. Kamati imebaini katika Kanuni hizi imeelezwa kuwa Waziri anaweza kuongeza orodha ya wanufaika wa mafao ya kuumia kazini. Hii inaleta utata wakati wa utekelezaji.

kwani ni wafanyakazi wa aina gani wanaopaswa kuengezwa ambao hawajatajwa ndani ya Kanuni hii.

2. Kamati imebaini katika Kanuni ya 6 inaeleza kuwa fedha za mfuko zinaweza kutumika kwa kuimarisha usalama na afya kazi, suala hili linaweza kuleta mgongano wakati wa utekelezaji kwani Idara ya Usalama na Afya Kazini ndio yenye jukumu la msingi kisheria, hivyo ni vyema kuliachia liwe linatekelezwa na mamlaka hiyo kikamilifu, badala ya kuachia kutekelezwa na mamlaka mbili tofauti, ili kuepusha mgongano wa kimajukumu.

3. Kamati imebaini kutokuainishwa kwa Kanuni ya muda maalum ambao mfanyakazi atakuwa amepewa mafao yake baada ya kutoa taarifa ya kuumia kazini.

4. Kamati imebaini changamoto kubwa katika Jadweli la 3 la Kanuni hiyo kwani kumekosekana kwa uwiano wa madhara yanayopatikana kulingana na viwango vya asilimia ya ulemavu wa kudumu kwa mwanachama wa mfuko, hali itakayopelekea kutopatiwa mwanachama huyo stahiki ipasavyo.

### 2.7.3 MAPENDEKEZO

Kamati inapendekeza kama ifuatavyo:

1. Kanuni ya 1, irekebishwe kwa kufutwa neno **“Mheshimiwa”**.
2. Kanuni 2(3), irekebishwe kwa kufutwa na kuunganishwa na Kanuni ya 1, kwani ni Kanuni inayozungumzia kuanza kutumika kwa Kanuni hizi ambayo, hiyo ni Kanuni ya 1, (commencement) kwa mujibu wa utaratibu wa uandishi (the Law of interpretation). Hivyo Kanuni ya 1 inarekebishwa kwa kuongeza Kanuni ndogo ya (2) na itasomeka kama ifuatavyo: **“bila ya kuathiri Kanuni ndongo ya (1) ya Kanuni hii malipo ya fao la kuumua kazini yataaza kulipwa kwa wafanyakazi kuanzia tarehe 1 Julai 2023”.** Aidha, marekebisho hayo yatapelekea Kanuni ya 1, kuwa “1-(1) …….”.
3. Kuangaliwa upya Kanuni ya 2 kwani Kanuni hiyo imeainisha wafanyakazi wanaopaswa kulipwa fao la kuumia kazini ni wanachama wote wa mfuko lakini Kanuni ya 2(4) inaeleza kuwa Waziri anaweza kujumuisha wafanyakazi wengine kupata Mafao ya Kuumia Kazini.
4. Kanuni ya 6(c) ifutwe kwani inaeleza matumizi ya fedha za Skimu ya Fidia kuwa miongoni mwa matumizi yake zitatumika kuimarisha uwepo wa usalama na afya kazini. Kamati imeona Kanuni hii inaweza kuleta changamoto hasa ikizingatiwa kuwa jukumu la kuimarisha usalama na afya kazini ni jukumu la Idara

ya Usalama na Afya Kazini ambayo iko chini ya Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji.

5. Kanuni ya 8(b) inarekebishwe kwa kufutwa maneno **“au ripoti”** kwa sababu yana maana moja.

Aidha, mapendekezo mengine yameainishwa katika **Kiambatanisho Namba 7** cha Ripoti hii.

### 2.7.4 USHAURI

1. Kamati inashauri kuwekwe muda maalum ambao mfanyakazi atakuwa amelipwa mafao mara baada ya kuumia.
2. Kamati inashauri jukumu la matibabu liondolewe kwa mwajiri kwani muajiri amechangia mafao hayo kwa mfuko kwa kila mfanyakazi wake.
3. Kamati inashauri Kanuni zirekebishwe kwa kukokotoa Fao la Kifo kwa miezi 36 badala ya miezi 48 iliyopo sasa ili kwenda sambamba kama ilivyo katika Sheria.
4. Kamati inashauri Mfuko kuweka miongozo itakayoweka utaratibu wa kuyataumbua maradhi yatokanayo na kazi na asiliamia ya ulemavu ili kuweza kulipa fidia kulingana madhara yaliyopatikanwa kwa mwanachama huyo.

## 2.8 KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (FAO LA UPOTEVU WA AJIRA) 2022.

### 2.8.1 UTANGULIZI.

Kanuni hizi zimetokana na Sheria Namba 2 ya 2005 chini ya kifungu cha 44.

Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha kwa Fao la Upotevu wa Ajira kwani kuja kwa jambo hili limekuja kusaidia mwanachama walioathirika na upotevu wa ajira kufaidika na Fao la Upotevu wa Ajira ambapo nyuma kulikua hakuna Fao hilo.

Kamati imepitia Kanuni hizi kuangalia iwapo zimefuata taratibu cha uandishi wa kisheria na kuzingatia matakwa ya wanufaika wa Kanuni hizi.

Katika kupitia Kanuni hizi Kamati imebaini changamoto kadhaa Pamoja na kasoro za kiuandishi na hiyo kupendekeza marekebisho.

### 2.8.2 CHANGAMOTO

1. Kamati imebaini kuwa kuna changamoto ya uwasilishwaji wa **Fomu ya Maombi ya Mafao ya Upotevu wa Ajira** kwani inatakiwa kuwasilishwa na mwanachama na mwajiri, na kwa nini Fomu hii isiwasilishwe na upande mmoja tu.

2. Kamati imebaini ndani ya Jaduweli la Kanuni hii kumetumika maneno ya “**upotevu wa ajira”** na “**ukosefu wa ajira”** ambayo kimsingi yana maana tofauti.

3. Kamati imebaini Mfuko unaweza kumuhamisha mwanachama kutoka mfuko mmoja kwenda mwengine bila ya ridhaa ya mwanachama husika.

### 2.8.3 MAPENDEKEZO

Katika kuimarisha Kanuni hii Kamati inapendekeza yafuatayo:

1. Kanuni ya 2 neno "**mkurugenzi mwendeshaji"** linarekebishwa kwa kufuta maneno "**chini ya"** yaliopo mwishoni mwa mstari wa pili wa neno hilo.
2. Kanuni ya 4(2) inarekebishwa kwa kufuta neno "**mwananachama"** na kuweka badala yake neno "**mwanachama".**
3. Marekebisho mengine yameoneshwa katika **Kiambatanisho Namba 8,** ndani ya Ripoti hii.

### 2.8.4 USHAURI

1. Kamati inashauri kuwepo kwa mazingatio makubwa katika Kanuni ya 7 kuwekwa bayana maneno **"kipindi Fulani**" yaliojitokeza katika Kanuni hiyo ambayo hayana tafsiri moja na hivyo yanaweza kuleta utata.

## 2.9 TANGAZO LA KIMA CHA CHINI CHA MISHAHARA KATIKA SEKTA BINAFSI, 2023.

### 2.9.1 UTANGULIZI

Tangazo hili linatokana na Sheria Namba 11 ya 2005 chini ya kifungu cha 96.

Kamati imefarijika kuona kwamba Wizara imetambua umuhimu wa Sekta Binafsi, kwa kuweka kima cha chini kipya cha mshahara ili wafanyakazi wa hizo kunufaika kutokana na kima hicho cha chini. Aidha lengo la kutolewa Tangazo hilo ni kuendana na wakati wa hali halisi ya maisha ya sasa ya kiuchumi. Na kuondosha utofauti wa kipato baina ya Sekta Binafisi na Serikali.

Kwa ujumla Tangazo limeandikwa vizuri kwa kuzingatia taratibu za kiuandishi licha ya kwamba Maudhui ya Tangazo hilo yameasikisi ipasavyo kupitia Tangazo husika lakini bado kuna changamoto chache Kamati imebaini

### 2.9.2 CHANGAMOTO

1. Baadhi ya waajiri wa Sekta Binafsi wanaendelea kutoa taarifa za uongo katika mikataba ya watumishi ili kwenda kinyume na matakwa ya Tangazo hilo.

2. Kamati imebaini licha Tangazo kutolewa kuanzia tarehe 24, Machi, 2023 lakini bado utekelezaji wake kwa baadhi ya sekta hizo binafsi umekua mgumu haswa kisiwani Pemba.

### 2.9.3 MAPENDEKEZO

Kamati inapendekeza kama ifuatavyo:

1. Taasisi husika kuhakikisha kwamba inasimamia Tangazo hili kwa kutoa elimu kwa jamii, juu ya haki zao na fursa ambazo zimeanishwa katika Tangazo hilo kima cha chini cha Mshahara kwa lengo la kuinua kipato cha wafanyakazi wa Sekta Binafsi.

2. Taasisi husika kuwafuatilia waajiri katika sehemu zao za kazi mara kwa mara ili kuangalia mikataba wanaoingia baina yao na waajiriwa iwapo wamezingatia masharti ya Tangazo hilo kwa mujibu wa Sheria.

### 2.9.4 USHAURI

Kamati inaishauri Wizara kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Tangazo hili, kwani kuwa na Sheria nzuri ni jambo moja na utekelezaji wa Sheria ni jambo jingine Tofauti. Hivyo Wizara isimamie utekelezaji wa Tangazo hilo kwa Sekta hizo Binafsi.

## 2.10 KANUNI ZA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA 2023.

### 2.10.1 UTANGULIZI

Kanuni hizi inatokana na Sheria Namba 8 ya 2021, chini ya kifungu cha 84(2).

Kamati imepata fursa ya kupitia Kanuni hizi Pamoja na kukutana na Wadau kwa lengo la kuziimarisha na kuhakikisha kuwa iwapo utaratibu wa uandishi wa Sheria umefuatwa kikamilifu. Wadau hao waliweza kuanisha changamoto mbalimbali zilizomo katika Kanuni na zile ambazo zinatokea nje ya matakwa ya Kanuni. Waliweza kuzionesha changamoto hizo na miongoni mwa hizo ni kuwepo kwa mgongano wa majukumu baina ya Kanuni hizo na zile za Mkemia Mkuu wa Serikali.

Katika mapitio Kamati imejiridhisha kuwa Kanuni imefuata Taratibu za uandishi licha ya kuwepo kwa kasoro za msingi ambazo zimejitokeza wakati wa kupitia Kanuni hizo.

### 2.10.2 CHANGAMOTO

1. Kamati baada ya kuipitia kwa kina ili kujiridhisha kama Kanuni imeafuata utaratibu wa uandishi wa Kanuni kama ilivyolezwa mwanzoni mwa Ripoti hii, Kamati ilibaini kuwa Kanuni hizi zina changamoto ya muingiliano mkubwa wa majukumu ya kazi na Sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali

Zanzibar, Sheria nambari 10 ya mwaka 2011, na Kanuni za Kemikali za Viwandani na Majumbani za Mwaka 2014. Miongoni mwa changamoto hizo ambazo zimejitokeza katika Kanuni ya 7 hadi 29, zimeonekana kugongana kimajukumu na Kanuni za Kemikali za Viwandani na Majumbani za Mwaka 2014, zinazotokana na Sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar.

2. Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto katika Kanuni ya 4(2) inayozungumzia utekezaji wa dawa za Nakotiki, Saikotropiki na Kemikali Bashirifu ambapo katika Kanuni ndogo hiyo ya (2) Mamlaka imejipa uwezo panapokuwa na dharura baada ya kupata idhini ya Mahakama kuziteketeza dawa hizo bila kuwepo kwa wahusika waliotajwa katika Kanuni ndogo ya(1) ambapo jambo hilo ni kinyume na utaratibu wa kisheria kwani jambo hilo haliwezi kutekelezeka pasi na uwepo wa Mkemia Mkuu au Mwakilishi kwenye uteketezaji huo ambapo Kamati imeliona hilo kama ni mgomgano wa kimajukumu baina ya Taasisi mbili kati ya Mamlaka ya madawa ya kulevya Zanzibar na Ofisi ya Mkemia Mkuu Zanzibar.

3. Aidha Kamati imebaini katika Kanuni ya 4(1) kuwepo kwa upungufu wa kutozingatiwa mjumbe muhimu kutoka Mamlaka ya Mazingira (ZEMA) ambae yeye ndo mtaalamu atakaeweza kutoa tathmini ya eneo husika pamoja na

mazingira halisi na athari zitakazoweza kujitokeza na hatua za kuchukuliwa baada ya kujitokeza athari hizo.

### 2.10.3 MAPENDEKEZO

Kamati inapendekeza kama ifuatavyo;

1. Mamlaka kuandaa kikao na Taasisi zinozoguswa ndani ya Kanuni, miongoni mwa taasisi hiyo ni Mkemia Mkuu wa Serikali kwani kwa kiasi kikubwa majukumu yake yanagongana na kanuni hizo za Mamlaka. Kwa kuwa Mkemia mkuu ni mtekelezaji mkuu wa majukumu kwa upande wa kemikali bashirifu, hivyo Kamati inapendekeza kikao hicho kifanyike na Ripoti ya kikao hicho iwasilishwe kwa Kamati ili Kamati iweze kutoa maoni yake ya kisheria.

2. Kamati inapendekeza kwa Mamlaka wakati kutunga Kanuni kuzingatia kwamba wakati wa kutunga Kanuni haikiuki Misingi ya Katiba na pia Kanuni hiyo iwe haendi kinyume au kugongana na Sheria Mama au Sheria nyengine.

Kamati inapendekeza kwa Mamlaka kuzingatia maagizo mengine ya kiuandishi ambayo yameambatanishwa katika **Kiambatanisho Namba 9 ndani ya Ripoti** hii.

### 2.10.4 USHAURI

Kamati inaishauri Mamlaka kuhakiksha kwamba wakati wa kikao watachokifanya kati yao na Mkemia Mkuu wa Serikali, kuhakisha masharti ya uandishi wa Kanuni unazingatiwa, ili kuepusha mgongano wa kisheria na Kanuni zake na muingiliano wa majukumu katika Sheria nyengine.

## 2.11 KANUNI ZA UTUMISHI ZA MAMLAKA YA UTHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR, 2013.

### 2.11.1 UTANGULIZI

Kanuni hii inayotokana na Kifungu 16 (f) cha Sheria ya Mamlaka ua Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar, Namba 7 ya 2013, ambapo Bodi imepewa uwezo wa kisheria kutunga Kanuni hizo.

Katika kujiridhisha iwapo utaratibu wa kawaida wa utungaji wa Kanuni wa ushirikishwaji wa Wadau umefuatwa ndani ya Kanuni hizi. Kamati, ilifanya mahojiano na Taasisi husika ili kujiridhisha kwamba Wadau walipatiwa fursa ya kushiriki katika utungwaji wa Kanuni hizo. Aidha, Kamati ilibaini kwamba, ushirikishwaji wa Wadau kwa kiasi kikubwa ulizingatiwa kwani Wadau waliweza kuonesha maoni yao yalivozingatiwa ndani ya Kanuni hizo.

### 2.11.2 CHANGAMOTO

Katika kuifanyia uchambuzi Kanuni hii, Kamati imeona kwa ujumla Kanuni imezingatia matakwa ya uandishi wa kisheria, licha ya kwamba kuna kasoro chache za kiuandishi wa Kisheria. miongoni mwa changamoto hizo ni:

1. Kamati imebaini katika Kanuni hizo haikuzingztia suala la Elimu kwa wafanyakazi wanaoelekea kustaafu.
2. Aidha Kamati imebaini kutozingatiwa sharti liliyopo kwenye Kanuni ya Utumishi wa Umma kuhusu Mafunzo ya watumishi katika muda au kipindi ca majaribio ambapo ni jambo la msingi kupatiwa mtumishi huyo katika kipindi hicho cja majaribio.

### 2.11.3 MAPENDEKEZO

Kamati baada ya kupitia Kanuni hizo inapendekeza yafuatayo;

1. kuwekwa kwa Kanuni itakayozungumzia mafunzo kwa mfanyakazi anaelekea muda wa kustaafu.
2. Kuwekwa kwa Kanuni mpya inayozungumzia mafunzo ya watumishi katika muda au kipindi cha majaribio.

Kamati inapendekeza Mamlaka kuzingatia Marekebisho mengine ya kiuandishi ambayo yameambatanishwa katika **Kiambatanisho Namba 10** ndani ya Ripoti hii.

### 2.11.4 USHAURI.

Kamati inashauri yafuatayo:

1. Kupatiwa elimu watendaji wa Mamlaka juu ya uwepo wa Kanuni ya Utumishi ya Mamlaka.
2. Kanuni izingatie posho la mazingira magumu kwa wafanyakazi wa Mamlaka pamoja na kupatiwa Posho la sare watendaji kwani halikidhi mahitaji yao kwa mwaka.
3. Aidha suala la Kuzingatiwa kwa watu wenye mahitaji maalum wakati wote haswa katika kipindi cha muda wa majaribio ni jambo la kuangaliwa kwa kina kwani mara nyingi huwa wanakosa fursa hizi kutokana na kukosa vifaa kutokana na mahitaji yao.
4. Kwa kuwa Mamlaka ni Taasisi yenye nguvu na mambo yake mengi yanahitaji usiri zaidi hivyo ni busara kuwekwa Kanuni inayozungatia Posho la kutunza siri.

## 2.12 KANUNI ZA UHIFADHI NA UENDELEZAJI WA MJI MKOMGWE, 2023.

### 2.12.1 UTANGULIZI

Kanuni hii inatokana na Sheria Namba 4, 2010 chini ya Kifungu cha 37.

Kamati imepata fursa ya kupitia Kanuni hizi kwa lengo la kuhakikisha kuwa iwapo utaratibu wa uandishi wa sheria

umefuatwa kikamilifu. Aidha wakati Kamati inapotaka kutoa ushauri, utaratibu ni lazima yapatikane maoni ya Wadau husika, ili kuona kama Kanuni hiyo imetimiza matakwa ya uandishi wa Kanuni ya ushirikishwaji wao.

### 2.12.2 CHANGAMOTO

1. Kamati ilipata changamoto ya kutopata michango kutoka kwa Wadau kutokana na kucheleweshwa kupatiwa Kanuni hiyo kwa wakati.
2. Kamati ilikosa kukutana na Mamlaka husika ili kuwasilisha maoni juu ya Kanuni hiyo.

### 2.12.3 USHAURI.

a) Kanuni ya 5 maneno ya pembeni yafutwe na kuandikwa upya kama ifuatavyo "**ruhusa ya kuendeleza eneo la hifadhi**"

b) Kanuni zote za adhabu ya faini ziweke kima cha chini na cha juu.

c) Kanuni ya 8(1) neno **"yatamilikiwa"** lisomeke **"yatasimamiwa"**

d) Kanuni ya 10(1) haieleweki iandikwe vizuri

**e)** Kanuni ya 11 iwekewe ufafanuzi wa maneno **"maeneo ya msingi".**

f) Kanuni ya 12 iandikwe upya kama ifuatavyo **"majengo yote ya mji mkongwe yatawekwa katika madaraja kama ilivyoainishwa katika mpango mkuu wa uhifadhi"**.

g) 12(2) jadweli liainishwe kuwa ni la kwanza (1) pia uhifadhi uwe kwa mujibu wa Kanuni na sio uwezo wa Mamlaka.

h) Kanuni ya 15 neno "**iliyosainiwa"** lisomeke "**iliyothibithishwa"**.

i) Kanuni ya 19 iwekwe katika hali ya ummoja.

j) Kanuni ya 20. Eneo la Mji Mkongwe liwekwe katika ufafanuzi.

k) Kanuni ya 21. Kwakuwa Bati zina viwango vyake ni vyema iweke viwango hivyo.

l) Kanuni ya 24. iangaliwe vizuri ili kuepusha mgongano na Sheria ya Uchaguzi.

m) Kanuni ya 25. iangaliwe vizuri ili kuepusha mkongano na Sheria ya inayosimamia masuali ya vibali vya mziki

n) Kanuni ya 28. Neno **"Waziri**" liwe katika ufafanuzi.

o) Kanuni ya 30. iwekwe vizuri kama inahusu makosa yote au makosa maalumu. Na kama makosa maalum yawe yameainishwa vizuri.

### 2.12.4 MAPENDEKEZO

Kamati inapendekeza kwa Wizara kukamilisha utaratibu wa Kamati hii wa kukutana na Wadau na kufanya Majumuisho na Wizara kuhusu Kanuni hizi kwani Kamati bado haikukamilisha taratibu zake ili kuweza kushauri na kutoa mapendekezo yake

kwa ujumla kwa Wizara. licha kwamba Kamati tayari imeshafanyia mapitio ya Kanuni hii kwa kina lakini bado Kamati ina haki ya kujiridhisha utaratibu uliotumika katika kutunga Kanuni hizi na vipi maoni ya Wadau yameweza kuzingatiwa.

Hivyo Kamati inasisitiza Mamlaka ya Mji Mkongwe kujipanga tena kwa ajili ya kukamilisha hatua hizo.

## 2.13 KANUNI YA UDHIBITI WA HOSPITALI BINAFSI, 2023

### 2.13.1 UTANGULIZI.

Kanuni hizi zinatokana na Sheria Nambari 4/1994 chini ya Fifungu cha 26.

Kwa ujumla Kanuni imeandikwa vizuri kwa kuzingatia utaratibu wa uandishi wa Kisheria.

Hata hivyo Baada ya kuipitia Kanuni hiyo Kamati inashauri kufanyika kwa marekebisho katika baadhi ya Kanuni.

### 2.13.2 USHAURI

a) Tafsiri ya **"Daktari dhamani"**
b) Kanuni ya 6(a) ifutwe na iandikwe upya kama ifuatavyo**:**
   **"Hospiali kwa muda wote wa kazi awepo Daktari msimamizi"**.
c) Kanuni ya 6 (b) Maneno **"wa ajira"** yafutwe na kuweka badala yake **"wa usimamizi".**

d) iongezwe Kanuni mpya ya (f) kama ifuatavyo

**"Awepo dakatari dhamana wa Hospitali".**

e) Kanuni ya 7(2)(b) itoke. kwani maelezo hayo yameshaelezwa katika Kanuni za awali.

f) Kanuni ya 9(d) maneno "**wa ajira**" yatoke.

g) Kanuni ya 9(e) yaongezwe maneno "**ikiwa ni taasisi".**

h) Kanuni ya 13(f) ifutwe na kauandikwa upya kama ifauatavyo.

"**Muambaji ametiwa hatiani kwa kosa la jinai linalohusiana na rushwa, uhujumu Uchumi au maadili na kutumikia chuo cha mafunzo kwa muda usiopungua miezi sita**".

i) Kanuni ya 15 (2) (ii) irekebishwe na iwe kama Kanuni ya 13(f).

j) Kanuni ya 15 (2) iii) na iv) Maneno **"wahudumu wa afya"** yaangaliwe vyema kama ndiyo yaliyokusudiwa.

k) Kanuni ya 15(4) Kibali kinatolewa na Bodi lakini kinafutwa na Waziri. hii haipo sawa iangaliwe tena.

l) Kanuni ya 18(2) maneno "**wa ajira"** yafutwe na kuweka badala yake **"wa usimamizi'.**

m) Kanuni ya 18 (2) "f" itoke.

n) Kanuni ya 30(2) (f) itoke.

o) Kanuni ya 55 maneno ya pembeni yasomeke **"kuondoa na kubakiza".**

### 2.13.3 MAPENDEKEZO

Kamati inapendekeza Wizara kupitia Kanuni ya **UDHIBITI WA HOSPITALI BINAFSI,2023,** kukamilisha utaratibu wa Kamati hii wa kukutana na Wadau kwa upande wa Pemba kwani Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wadau hao ambao wote kwa ujumla walikuwa hawajapatiwa nakala ya Kanuni na wala hawazitambui Kanuni hizo, ambapo Kamati ilitoa maelekezo kwa Wizara kuandaa kikao chengine ili Wajumbe wa Kamati kukutana na Wadau kwa upande wa Pemba ambao walishiriki kikamilifu katika kutoa maoni yao juu ya Kanuni hizi pamoja na kukamilisha utaratibu wa kufanya Majumuisho na Kamati hii kuhusu Kanuni hizi. Kwani Kamati bado haikukamilisha taratibu zake ili kuweza kushauri na kutoa mapendekezo yake kwa ujumla kwa Wizara. licha kwamba Kamati tayari imeshafanyia mapitio ya Kanuni hizi kwa kina lakini bado Kamati ina haki ya kujiridhisha utaratibu uliotumika katika kutunga Kanuni hizi na vipi maoni ya Wadau yameweza kuzingatiwa.

## SEHEMU YA TATU

### 3.1 HITIMISHO

Kamati inaimani kuwa Serikali itayafanyia kazi mapendekezo yaliyomo katika Ripoti hii na maoni yatakayotolewa na Wajumbe wa Baraza ili kuondoa dosari zilizobainika kutokana na uchambuzi wa Kamati katika Kanuni husika.

Kamati inashauri Wizara, Mamkala, Mashirika na Taasisi zote kwa ujumla ambazo zimekasimiwa madaraka hayo na Baraza la Wawakilishi kuhakikisha kwamba Kanuni zao walizokwisha kuzitunga au wanazotarajia kuzitunga waziwasilisha katika Kamati hii ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ambayo kwa niaba ya Baraza la Wawakilishi ina jukumu la msingi kuhakikisha Kanuni zote pamoja na Sheria ndogo ndogo hazijatoka nje ya mipaka na zimefuata utaratibu kikamilifu ili dhana ya kukasimu madaraka iweze kufikiwa kwani endapo kutakuwa na dhana ya kukasimu madaraka kunaenda sambamba na usimamizi wa madaraka hayo.

Pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa kila Taasisi zenye Kanuni hapo juu, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kama ifuatavyo:

a) Serikali ihakikishe Kanuni zinatungwa kwa wakati ili utekelezaji wa Sheria ufikie malengo yaliyokusudiwa;

b) Ushirikishwaji wa Wadau na wahusika wengine ufanyike katika hatua za uandishi wa Kanuni;

c) Kutolewe Elimu kwa Umma kabla au wakati Kanuni zinatungwa ili wananchi wafahamu utekelezaji wa Kanuni badala ya kuwashtukiza;

d) Serikali iweke muongozo wa utunzi (draft manual) ili kuwe na muelekeo unaofanana wa Kanuni (consistency);

e) Marekebisho ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria yafanyike haraka ili kuwa na sheria inayokwenda na mahitaji ya hivi sasa.

**3.2 MWISHO**

Kamati inapenda kutoa shukurani kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa ushauri, miongozo na maelekezo mbali mbali katika kutekeleza kazi za Kamati kwa ufanisi mkubwa na kutuwezesha leo kuwasilishwa Ripoti yetu katika Baraza lako tukufu. Ni matumaini yetu kuwa, utaratibu huu utakuwa endelevu kwa Kamati zote katika maendeleo ya nchi yetu.

Aidha Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo na kuiwezesha Kamati yetu kufanya kazi zake vizuri.

Kipekee kabisa naomba nimshukuru Mhe. Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma

na Utawala Bora pamoja na Mhe. Dr. Mwinyi Haji Talib (Mwanasheria Mkuu) wote kwa pamoja walishirikiana nasi kupitia Maafisa wao kufanikisha majukumu yetu kwa urahisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wakuu wa Sekta mbali mbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Kamati.

## VIAMBATANISHO VYA RIPOTI YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO YA BARAZA LA WAWAKILISHI

### KIAMBATANISHO NAMBARI 1

### KANUNI ZA BENDERA NA NEMBO YA MAHAKAMA, ZANZIBAR

Kamati baada ya kupitia Kanuni hii kwa kina pamoja na kukutana na watendaji wa Taasisi mbali mbali zinazosimamia masuala ya Bendera na Nembo, ilibaini kasoro katika Kanuni hizo. na changamoto mbali mbali, miongoni mwa mapendekezo ya Kamati ni pamoja na:

- Kanuni haikuweka Kanuni za adhabu kwa mtu anayekiuka masharti yaliyowekwa na Kanuni.
- Kanuni haijazingatia vipimo vya rangi za Bendera na Nembo.
- Kanuni haijazingatia vipimo vya ukubwa wa Bendera na Nembo.
- Kanuni haijaweka utaratibu wa uteketezaji pindi ikiwa haiwezi kutumika tena.

Mbali na hayo Kamati ilipata fursa ya kupitia Kanuni hiyo na kubaini mambo yafuatayo:

- Kanuni ya 1, kuhusu **Jina fupi.** Maneno **"utawala wa Mahakama"** yatoke na kuweka Neno "**Kanuni"**
- Kanuni ya 2. kuhusu Tafsiri, ya **"Bendera ya Mahakama".** Lifanyiwe tafsiri neno **"Bendera"**
- Kanuni ya 2. Mpangilio wa Maneno yaliyotafsiriwa, uwekwe kwa mpangilio wa alfabeti.
- Kanuni ya 2. kuhusu Tafsiri, ya **"Afisa wa Mahakama"** maneno hayo yafanyiwe tafsiri kwa mujibu wa sheria husika ya utawala wa mahakama nambari 11 ya 2018.

- Kanuni iongezwe Kanuni ya 3 iwe inahusu **“Matumizi”** ieleze Kanuni itatumika kwa nani au wapi.
- Kanuni ya 3, inahusu Bendera ya Mahakama, Maneno ya pembeni yasomeke “**Bendera na Nembo ya Mahakama ya Zanzibar”**
- Kanuni ya 3 yaongezwe mwisho wa Kanuni hii Maneno **“kama zilivyoainishwa katika jadweli la Kanuni hizi.”**
- Kanuni ya 3(2) Bendera ielezwe rangi na umbo lake kwa kutumia vipimo, ielezwe katika jadweli (**specification).**
- Kamati inataka ufafanuzi wa Kanuni ya 5, kuhusu Jaji Mkuu kupeperushi bendera katika gari.
- Aidha, Kamati inataka ufafanuzi juu ya Makaazi rasmi. Je ipo nyumba rasmi ya jaji Mkuu? Au anaamua mwenyewe makaazi rasmi.
- Kanuni ya 6, neno “**kutundika”** liwe “**kuweka”**
- Kanuni ya 9 iandikwe upya kama ifuatavyo:

  “**Kila Afisa wa Mahakama atawajibika kupeperusha bendera safi, haijachanika, kuchakaaa au kuharibika kwa namna yoyote ile”.**
- Iongezwe Kanuni ya 12 mpya ieleze **“uteketezaji wa bendera isiyofaa kwa matumizi”**. Mtendaji Mkuu wa Mahakama atandaa utaratibu wa kuteketeza bendera na Nembo isiyofaa.
- Kanuni iweke utaratibu wa kupeperusha bendera panapokuwa na bendera nyingine hasa katika shughuli za kitaifa.

**MAKOSA NA ADHABU.**

Kanuni Haikuwekewa kanuni za makosa na adhabu kwa atakaekiuka masharti yaliyomo katika Kanuni hii. Ni vyema baadhi ya masharti yawekewe kanuni za makosa na adhabu.

Miongoni mwa makosa hayo ni kama:

a) **Mtu yeyote atakayechana au kuchoma moto bendera kwa nia ovu atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia…………………**

b) **Mtu yeyote akayepeperusha au kuweka mezani bendera hali ya kuwa hastahiki kisheria kufanya hivyo atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia……………………………**

c) **Mtu yeyote atakayepeperusha au kuweka mezani bendera iliyochanika atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia …………**

**NAOMBA KUWASILISHA**

…………………………………

**Mihayo Juma N'hunga**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar**

**KIAMBATANISHO NAMBARI 2**

## KANUNI ZA WAFANYAKAZI ZA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

## UTANGULIZI

## HALI HALISI KUHUSU KANUNI ZA WAFANYAKAZI ZA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR

Kamati imepokea na kupitia KANUNI ZA WAFANYAKAZI WA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR, baada ya kupitia Kanuni hiyo Kamati imebaini yafuatayo:

Kanuni husika iliyowasilishwa katika Kamati haionekani kama ilitangazwa katika ***Gazeti Rasmi la Serikali jambo ambalo ni sharti la lazima kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 36 na 37 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, nambari 7/1984.***

Hivyo, kwa kuzingatia utaratibu wa kisheria kilichowasilishwa mbele ya Kamati si Kanuni bali ni Rasimu ya Kanuni ambayo inatarajiwa kukamilisha utaratibu ili iwe Kanuni.

Kwa msingi huo suala hili kuwasilishwa katika Kamati wakati wake bado (immature) na kama wakati wake bado Kamati haina jukumu ya kuifanyia kazi, hata hivyo kwa dhamira ya kuisaidia Taasisi Kamati imeona ni busara kutoa ushauri ili itakapowasilishwa Kanuni hii iwe imezingatia hoja ya maoni na ushauri wa Kamati.

Hivyo, Kamati iliona ni vyema kujielekeza katika kutoa ushauri wa jumla na sio kwenda Kanuni kwa Kanuni kwani Kamati inatarajia kuiona tena Kanuni hii ambayo itakuwa **imetimiza Utaratibu wa Masharti ya Uandishi wa Kisheria** ili iweze kupitiwa kuanzia Kanuni zinazozungumzia **Masharti ya Awali** hadi Kanuni ya mwisho ambayo inaondoa **Kanuni ya Awali na Kubakiza Kanuni hii (Revoke and Replace).** Aidha, inapendekeza yafuatayo:

i. PBZ Wawasilishe mbele ya Kamati, Kanuni iliyotangazwa kisheria badala ya Rasimu ya Kanuni.

ii. Katika jina refu la Kanuni iweke kifungu kinachoipa mamlaka Bodi kuanzisha Kanuni hizi. (Enable Provision).

iii. Kuiona Katiba ya Benki ili kujiridhisha na Mamlaka ya Utungaji wa Kanuni.

iv. Kanuni itakayowasilishwa ifuate utaratibu wa uandishi wa Sheria kwani rasimu iliyowasilishwa imekosa kufuata **Mfumo wa Uandishi wa Kanuni** ama Sheria kwani Uandishi wa Sheria unakuwa katika uandishi wa vifungu **(Provision).** Hata hivyo Kanuni hii inaonekana ipo zaidi katika simulizi au maelezo (narration).

v. Kanuni imetumia Vichwa vya Habari (**Head note)** badala ya maneno ya pembeni (**Maginal note)** ieleweke kwamba kila nchi inayo utaratibu wa uandishi wake wa Sheria (indoor policy) ambayo hulazimika kufuatwa utaratibu wa ndani ambapo rasimu ya kanuni hii upo tofauti na ilivyoandikwa.

- Mfano **Sehemu ya Kwanza** mara nyingi huwa inabeba
- **MASHARTI YA AWALI (PRELIMINARY PROVISIONS)**

  1.Jina Fupi na Kuanza Kutumika,
  2.Matumizi ya Kanuni,
  3.Ufafanuzi wa Maneno,

Ambapo katika Kanuni hizi sehemu hii haijaonesha mambo hayo tu ya msingi, bali imesheheni maelezo ambayo mengine hayapaswi kuwepo katika sehemu hiyo mfano Kanuni ya kuondoa Kanuni hizi, Ambapo ipo katika Sehemu ya Kwanza (1.1) ambapo kwa kawaida hukaa katika Kanuni za mwisho (masharti mengineyo) na yalipaswa kusomeka kama ifuatavyo:

***a) kanuni za wafanyakazi za mwaka 2001, zinaondolewa,***
***b)Bila ya kuathiri kuondolewa kwa kanuni hizo jambo lolote halali lililofanywa au lililoachwa kufanywa na***

***kanuni zilizoondolewa litazingatiwa kuwa kimefanywa na kanuni hizi.”***

Aidha, katika Rasimu hii ya Kanuni maelezo ambayo hayakukaa katika sehemu zake au hayapaswi kuwepo kwa kuwa mengine sio sehemu ya Kanuni yanaonekana katika Kanuni zifuatazo (1.0), (1.1), (1.3), (1.5) (1.6).

**vi.** Kanuni hii ilihitajika kuainishwa **Sehemu ya Pili** ambayo inachukua dhana nzima ya **Uongozi wa Benki ya PBZ**.

Uongozi ambao utakuwa na wajibu wa kusimamia wafanyakazi kupitia Kanuni hizi kwa mfano:

- Bodi ya Wakurugenzi, (kuanzishwa, muundo na majukumu yake)
- Kamati ya Uongozi, (kuanzishwa, Muundo na majukumu yake)
- Na vyombo vyengine kadri itakavyoonekana inafaa

**vii.** **Sehemu ya Tatu** ielezee taratibu za uajiri na upandishwaji wa vyeo watumishi kwa kuzingatia Muundo wa Utumishi wa Taasisi ambao inatakiwa Bodi iandae kama jukumu lake la msingi, katika kusimamia haki za wafanyakazi.

- Bodi iandae utaratibu na kuweka bayana baina ya utaratibu wa uajiri wa watumishi wa kudumu na wa mikataba.

- Bodi katika kutekeleza majukumu yake ya kiitumishi inawajibika kuzingatia muongozo wa Sheria Namba 2 ya mwaka 2011.

Vilevile, **Sehemu ya Nne** ielezee wajibu na haki za wafanyakazi
Kwa kuzingatia wajibu wa kufanya kazi kwa bidii na uadilifu wa hali ya juu na kuweka mbele maslahi ya Taasisi.

Aidha, Kanuni izingatie kuwa Banki ni Taasisi ya kibiashara yenye ushindani hivyo utaratibu wa maslahi ya wafanyakazi ikiwemo mishahara, posho na maslahi mengine yazingatiwe kwa upekee, bila ya kusahau kwamba endapo mfanyakazi atakiuka masharti ya kinidhamu yatakayowekwa ndani ya Kanuni hizi au yaliowekwa ndani ya Sheria ya Utumishi wa Umma atawajibishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi na Kanuni hizi.
Pia Kanuni ieleze kwamba itasomwa sambamba na Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mwisho kabisa, Kamati inashauri Kanuni hii ingeliweza kujielekeza katika mambo ya msingi ya watumishi badala ya kuchukua kila kitu kilichokwisha kuwepo katika Kanuni ya Utumishi wa Umma na badala yake ijielekeze kwa mambo mahsusi ambayo yana maslahi na Taasisi bila ya kuathiri Sheria ya Utumishi wa Umma.
Bila ya kusahau, Kanuni imeweka fasili ya wafanyakazi ambayo imewaondoa Wajumbe wa Bodi.

Hata hivyo Wajumbe hao wanaonekana kupata maslahi kama watumishi kupitia Kanuni hii jambo ambalo sio sahihi kuwapa maslahi Wajumbe hao kupitia Kanuni hizi za Wafanyakazi. Kamati inashauri kuwekewa miongozo yao mbali na Kanuni hizi za Utumishi.

Mwisho kabisa. Kamati inashauri kwamba Kanuni hii kwa ilivyo haiwezi kuwasaidia walengwa kwa sababu haijatimiza masharti ya Kanuni kuwa Kanuni kwa mujibu wa Sheria na kwamba haiwezi kusimama kama nyaraka ya kisheria mbele ya vyombo vya Sheria kama Mahakama.

Aidha, Kanuni hii ifanyiwe mapitio kupitia Wataalamu wa Uandishi wa Sheria ili kuhakikisha Kanuni inaandikwa kwa lugha rahisi ya kisheria na katika utaratibu unaokubalika hasa kwa kuzingatia kwamba Kanuni hii imabeba maslahi mapana ya wafanyakazi.

Vilevile, Kamati inashauri kushirikishwa kikamilifu walengwa wa Kanuni hii kwani imebainika kwamba. Aidha, Wadau wa Kanuni hii hawakushirikishwa au maoni yao hayakuzingatiwa.

**NAOMBA KUWASILISHA KWA HATUA ZAKO**

**…………………………………**
**Mihayo Juma N'hunga**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar**

**KIAMBATANISHO NAMBARI 3**

**KANUNI ZAWAFANYAKAZI WA SHIRIKA LA BIMA 2023**

Kwanza kabisa Kamati inapongeza Shirika la BIMA kwa kuona umuhimu wa hali ya juu kuondolewa (To Revoke) Kanuni ya Utumishi ya Shirika la BIMA Zanzibar na kuwekwa mpya, sambamba na kutambua mambo yote yaliofanyika katika Kanuni iliyopita yanachukuliwa kuwa halali chini ya masharti ya Kanuni hii.

Aidha, Kamati inapongeza kwa kuona kwamba Kanuni hizi kwa kiasi kikubwa zimezingatia utaratibu wa uandishi wa kisheria licha ya kwamba katika kila uandishi wa kisheria hakukosekani kasoro. Kamati hii inajukumu la kuhakikisha kasoro hizo za kisheria na kimantiki zinawekwa sawa. Na hapo ndipo uwepo wa dhana ya kukasimu madaraka unatekelezwa kwa kuwepo usimamizi wa aliyekasimiwa ili kuona kwamba aliyekasimiwa hakuwa nje ya mipaka ya kisheria.

Baada ya utangulizi mfupi Kamati inapenda kutoa maoni yake juu ya Kanuni hii ya Utumishi ya BIMA.

Utaratibu wa kutunga Kanuni upo kisheria jambo la kuzingatia Kanuni yoyote inayotungwa ni lazima itokane na Sheria na anayetunga awe amepewa Mamlaka hayo na Sheria husika ni lazima kiwepo kifungu wezeshi (enable provision) kinachotoa maelekezo ya kutungwa kwa Kanuni na kutoa Mamlaka kwa mtunzi wa Kanuni. Bila ya kutimizwa kwa masharti hayo Kanuni inayotungwa huwa ni **batili tokea awali (void ab initio)**

Kamati imebaini kuwa Kanuni za Utumishi za Shirika la BIMA zimetungwa kutokana na ***kifungu cha 26(1)(a) cha Sheria namba 6 ya mwaka 2021.*** Hata hivyo baada ya kufanya mapitio katika Sheria hiyo kifungu

kilichoainishwa hapo kinazungumzia **kazi ya Bodi ya kutunga Sera ya Taasisi ya Uwekezaji wa Umma** na wala hakizungumzii kutungwa kwa Kanuni. Hivyo Kamati inaomba kupata ufafanuzi juu ya uwezo wa Bodi kutunga Kanuni hizi. Hata hivyo Kamati ilifanya kazi ya ziada ili kujiridhisha iwapo kuna kifungu chochote kinachoipa Mamlaka Bodi kutunga Kanuni. Kamati imebaini kifungu cha 26(1)(n) kimezungumzia masuala ya Kanuni lakini hakikuipa Bodi Mamlaka ya kutunga Kanuni bali imeipa Mamlaka Bodi kuidhinisha (approve) Kanuni. **Suala la kujiuliza je iwapo Bodi inaidhinisha ni nani anayeandaa Kanuni hizo na kupendekeza kwa Bodi ili iidhinishe kama vile ilivyo katika Sheria ya Utumishi kifungu cha 25(o) ambapo Mamlaka za kiutumishi huandaa Miundo na kuwasilisha Kamisheni ya Utumishi kwa kuidhinishwa. (Kamati inaomba kupatiwa ufafanuzi).**

mbali na utangulizi huo ambao unatakiwa kutolewa ufafanuzi Kamati iliona ni vyema kutekeleza jukumu lake la kupitia Kanuni hizi na imekuja na maoni yafuatayo

Kamati imeipitia Kanuni hii kwa undani kabisa na kugundua kasoro zifuatazo:

- Kawaida ya uandishi wa Kanuni lazima uandishi wa kichwa cha habari cha Kanuni kusika kutangulie Sheria ambayo ilitoa Mamlaka ya utungwaji wa Kanuni husika kama ifuatavyo:

“***SHERIA YA MSAJILI WA HAZINA***

***NAM.6 YA 2021***

***KANUNI YA UTUMISHI YA SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR***

***Chini ya kifungu26(1)(a)”***

Aidha, maneno uwezo wa utungwaji wa Kanuni hii ndio yanafuatwa.

Kamati inashauri kwenye sehemu ya kwanza kufuta maneno **"Utangulizi"** na badala yake kuandika upya maneno **"Masharti ya Awali"** chini ya maneno sehemu ya kwanza ili Kanuni iwe imefuata utaratibu wa uandishi wa kisheria.

Kamati inashauri kwenye Kanuni ya 1 kuweka maneno ya pembeni yanayosomeka kama ifuatavyo:

**"Jina fupi na kuanza kutumika"** badala ya maneno **"jina na tarehe kuanza kutumika"**

Kwenye Kanuni hii inatakiwa ionekane jina refu la Kanuni, Kanuni itaanza kutumika muda gani, baada ya kutiwa Saini na nani na kama itatangazwa kwenye Gazeti basi litajwe Gazeti Rami la Serikali. ***Kama inavyoshurutishwa katika kifungu cha 36 na 37 cha Sheria ya Ufafanuzi Nam.7 ya 1984.***

1. Kamati inashauri katika Kanuni ya 2 ya ufafanuzi wa maneno
    - ✓ "**Tafsiri ya Maneno"** ambayo kawaida huwa maneno ya pembeni yanapaswa kufutwa na kuandikwa **"Ufafanuzi".**
    - ✓ Neno **"Bodi"** lifanyiwe tafsiri kisheria.
    - ✓ Neno **"Rais"** lifanyiwe tafsiri

2. Kamati inashauri katika Kanuni ya 3, inarekebishwa kwa kuanza maneno kama yafuatayo:

   “3. (1) **kutakuwa na uongozi wa Shirika ambao utakuwa kama ifuatavyo**:”

Kamati inataka ufafanuzi katika Kanuni ya 5 kuhusu utaratibu wa vikao na majukumu ya Kamati hiyo kwa nini hayakuainishwa.

Kanuni ya 6 (1)(e) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“jinsia na”** kwani kuzingatia jinsia kunahitaji uwepo wa kuchagua watu wakianzia wawili.

Kanuni ya 6 (1)(f) inarekebishwa kwa kufuta neno **“ambae”**

Kanuni ya 8(1) inarekebishwa kwa kufuta neno **“zitakazoletwa mbela”** yaliopo baina ya neno **“zote”** na **“ya”** na kuweka badala yake maneno **“zitakazowasilishwa mbele”**

Kanuni ya 8(2)(a) inarekebishwa kwa kufuta neno **“kutoka”** yaliopo baina ya neno **“mwenyekiti”** na **“Idara”** na kuweka badala yake maneno **“ambaye atakuwa Mkuu wa”**

Kamati pia inapendekeza kuwa **Mkurugenzi Rasilimali Watu** kuwa mwenyekiti wa kamati hiyo.

Kanuni ya 8(2) (c) inarekebishwa kwa kufuta neno **“Mwasheria”** yaliopo mwanzoni mwa ayaya kanuni hiyo na kuweka badala yake maneno **“Mwanasheria wa Shirika”**
Pia Kamati inashauri kuwekwa vyema aya ya (c) kwani maneno **“nje au ndani”** hayapo wazi (uncertain).
Kanuni ya 9 inarekebishwa kwa kufuta neno **“maamuzi”** na kuweka badala yake maneno **“uamuzi”**.
Kanuni ya 9 inarekebishwa kwa kuongeza **“Utumishi wa Umma”** mwishoni mwa Kanuni hiyo. Kamati imeona kwamba kwa mujibu wa Kanuni hii ya Shirika la BIMA Sheria tayari ishafanyiwa tafsiri katika Kanuni ya 2.

Kanuni ya 11(1) inarekebishwa kwa kufuta neno **“Msajili wa Hazina nambari 6 ya mwaka 2021”**
Kanuni ya 11(2) inarekebishwa kwa kufuta na kuiandika upya na kusomeka kama ifuatavyo “**bila ya kuathiri masharti ya Kanuni ndogo ya (1) ya Kanuni hii, Bodi inaweza kukasimu madaraka yake kwa Mkurugenzi Mwendeshaji”**
Kanuni ya 12 inarekebishwa kwa kuweka **Proviso** mwishoni mwa Kanuni hiyo na kusomeka kama ifuatavyo **“katika utekelezaji wa ajira Bodi itapaswa kufuata masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Kanuni zake na Kanuni hizi.”**

Kanuni ya 13(d) inarekebishwa kwa kufuta neno **“kwa mujibu wa Sheria”** na kuweka badala yake maneno **“Misingi ya Uajiri”.**

Kanuni ya 14(1) inarekebishwa kwa kufuta neno **“hiyo kwa mujibu wa Sheria”** na kuweka badala yake maneno **“iliyowazi”**

Kanuni ya 15(1) inarekebishwa kwa kufuta neno **“kufanya usaili wa maombi”** yaliopo baina ya neno “la” na “na” kuweka badala yake maneno **“kusimamia utaratibu wa ajira kama itakavyoelezwa”**

Kanuni ya 15(3) inarekebishwa kwa kufuta neno **“kuwaalika watendaji”** na kuweka badala yake maneno **“kumualika Mtendaji yeyote”**

Kanuni ya 15(4)(a) inarekebishwa kwa kuongeza maneno **“kupekua na”** mwanzoni wa aya hiyo.

Kanuni ya 15(4)(c) inarekebishwa kwa kufuta neno **“ripoti”** na kuweka badala yake neno **“taarifa”**

Kanuni ya 17 inarekebishwa kwa kufuta neno **“au”** na kuweka badala yake **“,” baina ya neno “mwaminifu” na “uadilifu”**

Kanuni ya 18(1) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“vyovyote itakavyokuwa”** yaliopo baina ya neno “mwendeshaji” na **“endapo”**

Kanuni ya 18(2) (c) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“mobile za”** na kuweka badala yake maneno **“mbili zenye ukubwa wa”** baina ya maneno **“picha” na “pasi”**

Kanuni ya 18(4) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“upimaji wa afya”** na kuweka badala yake maneno **“Uchunguzi Afya Mfanyakazi”.**

Kanuni ya 19(1) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“kifungu**
**namba nambari”** na kuweka badala yake maneno **“Kanuni ya”**

Kanuni ya 19(1) inarekebishwa kwa kuingiza maneno **“kama ulioelezwa katika Jadweli la Tatu la Kanuni hizi”** baina ya neno **“ajira” na “mara”.**

Kanuni ya 21(1)(a) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"inayotumika Zanzibar"** na kuweka badala yake maneno **"ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya 2011"**
Kamati inataka kufahamu Kanuni gani iliyotoa mazingira ya ajira ya muda.
Kanuni ya 22(3) inafutwa na kuandikwa upya na kama ifuatavyo: **"Mfanyakazi akiwa katika muda wa majaribio atawajibika kwa Mkuu wa Idara inayohusika na atatakiwa kufuata masharti yote ya ajira kama mfanyakazi wa kawaida"**

Aidha, Kanuni ya 22 inarekebishwa kwa kuongeza Kanuni ndogo ya (5) na kusomeka kama ifuatavyo: **"Mfanyakazi akiwa katika muda wa majaribio atapatiwa mafunzo ya awali kabla kuthibitishwa kazi"**
Pia, Kanuni ya 22 inarekebishwa kwa kuongeza Kanuni ndogo ya (6) na kusomeka kama ifuatavyo: **"Mfanyakazi akiwa katika muda wa majaribio hatoruhusiwa kujiunga na masomo ya muda mrefu".**
Kanuni ya 24(1) inarekebishwa kwa kuingiza maneno **"Mkurugenzi Mwendeshaji"** baina ya neno **"na"** na **"atawasilisha"**
Kanuni ya 25(6) inarekebishwa kwa kuongeza maneno **"au aliyepata maradhi" Kamati imebaini kwamba kuna**

**umuhimu kwa mfanyakazi aliyepata maradhi kipindi cha majaribio naye azingatiwe.**

Kanunya 26 kuongezwe Kanuni ndogo (3) na (4) ambazo zitazungumzia utaratibu wa muda wa kuazimwa mfanyakazi pamoja na kuwekwa mazingira ambayo yatazuia shirika kumsomesha mfanyakazi huyo mafunzo ya muda mrefu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

Kanuni ya 27(1) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"kuidhinishwa na Mamlaka husika za Serikali"** yaliopo baina ya neno **"na"** na **"muundo"** na kuweka badala yake maneno **"kwa ajili ya kupendekeza na kuwasilisha kwa Mamlaka husika kwa kuidhinisha"**

Kanuni ya 27(2) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"bila ya kuathiri masharti ya Kanuni ndogo ya (1) ya Kanuni hii"** Kamati inashauri kuondolewa maneno hayo kwa sababu kuwepo kwake hakuleti maana.

Kanuni ya 28(1) inarekebishwa kwa kuingiza nambari na maneno **"27 ya Kanuni hizi"** baina ya neno **"ya" na "katika"**

Kanuni ya 28(12) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"endapo Mkurugenzi au Bodi itakapoona inafaa"** yaliopo mwanzoni mwa Kanuni hiyo. Aidha, kuingiza maneno

“katika nafasi aliyopandishwa” baina ya neno “yake” na “iwapo”.

Kanuni ya 28(4) inarekebishwa kwa kufuat maneno **“Mkurugenzi Mwendeshaji”** yaliopo baina ya neno **“hayaridhishi” na “atachukua” na kuweka badala yake neno “Bodi”**.

Kanuni ya 29(2) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“vyovyote itakavyokuwa”** yaliopo baina ya neno “mwendeshaji” na “atateua” na kuweka badala yake maneno “au Bodi”.

Vile vile, kuingiza maneno **“katika nafasi aliyopandishwa”**

Kanuni ya 34(3) inarekebishwa kwa kufuta neno **“kazi”** yaliopo mwishoni mwa Kanuni hiyo na kuweka badala yake maneno “utumishi wa umma”**.**

Kanuni ya 37(4) Kamati inashauri kuandikwa kwa ummoja badala ya wingi kwani kiuandishi wa sheria **(singler means prural)**

Kanuni ya 47(3) na 47(4) Kamati inahitaji ufafanuzi wa Kanuni hizo. Aidha, Kamati inashauri kutumia Kanuni badala ya kifungu pia maneno bila kuathiri bado yana utata katumika ndani ya Kanuni 47 ya Kanuni hizi.

Kanuni ya 48(2)(e) Kamati inataka kufahamu kwa nini Kanuni ya Utumishi wa Shirika izungumzie kuhusu Mwenyekiti wa Bodi.

Kanuni ya 51 inarekebishwa kwa kufuta maneno **"bila ya kuathri masharti ya Kanuni hii".**

Kanuni ya 57(2) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"kwa ajili ya kifungu hiki"** yaliopo mwanzoni mwa Kanuni hii na kuweka badala yake maneno **"kwa kuzingatia mashari ya Kanuni hii"**

Kanuni ya 58(2) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"kinyume chake"** yaliopo mwishoni mwa Kanuni hii. Kamati imeona uwepo wa maneno hayo hayana sababu ya kuwepo kwani Kanuni ilikuwa ishajitosheleza bila ya uwepo wa maneno hayo.

Kanuni ya 59(1) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"bila ya kuathiri kifungu cha Kanuni hii"** yaliopo mwanzoni mwa Kanuni hii.

Kanuni ya 60(1) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"Wajumbe wa Bodi"** yaliopo baina ya neno **"na"** na **"kwa"**. Kamati inashauri Wajumbe wa Bodi mambo yao yawekwe

katika miongozo yao na sio ndani ya Kanuni ya Utumishi ya Wafanyakazi.

Kanuni ya 64(2) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“miaka mitano mfululizo ya kujifunza jinsi ya kuishi akiwa mstaafu atakapofika umri wa kustaafu kwa lazima yaani miaka sitini”** na baada yake kuweka neno **“kazi”.**

Kanuni ya 65(3) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“kuachishwa kazi kwake”** na kuweka badala yake maneno **“kustaafishwa kazi”**

Kanuni ya 65(4) inarekebishwa kwa kufuta neno **“kuachishwa”** na kuweka badala yake neno **“atastaafishwa”**

Kanuni ya 69(2) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“kulipwa mafao yoyote”** kamati inashauri kufutwa maneno hayo kwani mfanyakazi huyo anayo haki ya kulipwa mafao yake aliyochangia katika ZSSF akifika umri wa kustaafu.

Kanuni ya 71(1) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“katika jadweli la Kanuni hizi”** na kuweka badala yake maneno **“katika jadweli la kwanza la Kanuni hizi”.**

Kanuni ya 71(2) inarekebishwa kwa kufuta neno **“atapoteza haki zake zote”** Kamati inashauri kwamba kuangaliwa tena Kanuni hii kwani mfanyakazi huyo anastahiki mafao aliyochangia baada ya kufika umri wa kustaafu.

Kanuni ya 73(2) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“Wajumbe wa Bodi”** yaliopo mwanzoni wa Kanuni hiyo. Ushauri wa Kamati ni ule ule Wajumbe wa Bodi wawekewe Utaratibu wao katika Miongozo ao na sio katika Kanuni ya Utumishi Umma ambayo walengwa ni watumishi wa umma. Aidha, marakabisho hayo yafanyike katika kila sehemu inapotaja wajumbe hao moja kwa moja haki zao ndani ya Kanuni hii

Kanuni ya 74(3) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“linaweza kugharamia”** liliopo baina ya neno **“shirika”** na **“usafirishaji”** na kuweka badala yake neno **“litagharamia”.**

Kanuni ya 82(1)(d). Kamati inashauri masharti ya Sheria ya ushiriki wa mfanyakazi katika siasa. “bila ya kuathiri masharti ya Kanuni ndogo ya(1)(e) ya Kanuni hii ikiwa mfanyakazi wa shirika anataka kujishirikisha katika siasa masharti ya Sheria ………yazingatiwe.” Kwa sababu wafanyakazi wapo katika madaraja tofauti kwa mujibu wa Sheria husika.

Pia, Kanuni haikuzingatia muda kwa washiriki wa masuala ya siasa ambapo kwa kawaida huwa ni vipindi vya miaka mitano ambapo kwa mujibu wa Kanuni ya Utumishi Kanuni ya 63(2) imetoa mazingatio kwa watumishi wanaoshiriki katika siasa.

Kanuni ya 87, Kamati inashauri kuweka tafsiri ya maneno “ndugu zake wa karibu kwani maneno haipo wazi.

Kanuni ya 89 inarekebishwa kwa kufuta maneno **“wa kiume”** yaliopo baina ya neno “mfanyakazi” na “atajifungua”.

Kanuni ya 96(2) inarekebishwa kwa kuingiza neno **“saba”** baina ya neno “la” na “la”.

Kanuni ya100(6)(1) inarekebishwa kwa kufuta namba “1” na kuweka badala yake neno **“kwanza”** baina ya neno **“la”** na **“la”.**

Kanuni ya 100(9) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“kifungu hiki”** liliopo baina ya neno **“na”** na **“atakuwa”**.na kuweka badala yake maneno **“Kanuni hii”**

Kanuni ya 112(1) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“nam.11 ya 2005”** yaliopo baina ya neno “ajira” na “yanayoeleza” na kuweka badala yake maneno **“Sheria ya Utumishiwa Umma nambari 2 ya 2011”** Kamati inashauri kutumika Sheria ya Utumishi kama inavyelezea katika kifungu cha 2 cah Sheria hiyo.

Kanuni 112(8) imefanya marejeo katika Sheria kwa mujibu wa Kanuni hii Sheria maana yake ni Sheria ya Hazina ambapo katika Sheria ya Hazina hakuna pahala ilipozungumziwa Bodi kuwa itakuwa ni chombo cha Rufaa hivyo Kamati inataka ufafanuzi.

Kanuni ya 116(3)(a)(b) katika Kanuni hii kuna neno **“Sheria”** kamati inashauri kuandikwe maneno **“SHERIA ya JINAI”**

Kanuni ya 131(1) kinarekebishwa

a) kwa kufuta maneno ya yanayojulikana ya pembeni **“kufutwa kwa Kanuni za 2017”** na kuweka badala yake maneno **“kuondolewa kwa Kanuni za 2017”.**

b) Kwa kufuta neno “**zimefuta”** na kuweka badala yake neno “zimeondoa” liliopo baina ya neno **“hizi”** na **“Kanuni”**

Kanuni ya 131(2) kinarekebishwa Kwa kufuta neno “**zilizofutwa”** na kuweka badala yake neno “**zilizoondolewa”** liliopo baina ya neno **“Kanuni”** na **“Kama”.**

**Naomba kuwasilisha**

**............................................**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

**KIAMBATANISHO NAMBARI 4**

**KANUNI ZA MASUALA YA WAZEE (UTOAJI WA HUDUMA ZA MAKAAZI) - ZANZIBAR**

1. Marekebisho katika Kanuni ya 3 ufafanuzi wa maneno
2. Neno **“Afisa”** tuliangalie iwapo limefanyiwa tafsiri katika Sheria tuhakikishe haikinzani na Sheria.

3. Neno “daftari la kumbukumbu” **“maana yake ni daftari maalum lililoanzishwa kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 7 ya kanuni hizi kwa dhamira ya kuweka kumbukumbu za usajili wa wazee.”**

4. Kuandikwa ufafanuzi wa neno **“muombaji**” **“maana yake ni mtu, taasisi inayokusudia kuanzisha makaazi ya wazee kupitia masharti ya sheria na kanuni hizi”**

5. Kuandikwa ufafanuzi wa neno **“Taasisi”** “**inajumuisha za Taasisi za Serikali au binafsi.”**

6. Katika kichwa cha habari katika jina la Kanuni linarekebishwa kwa kuongeza neno “**Zanzibar”** mwishoni mwa jina hilo**.**

7. Sehemu ya pili kichwa cha habari kinarekebishwa kwa kufuta maneno **“taratibu za usajili”** na kuweka badala yake maneno **“kuanzishwa kwa makaazi”**

8. Kanuni ya 4(1) inarekebishwa kwa kufuta na kuandikwa upya kama ifuatavyo **“kutakuwa na makaazi yatakayomilikiwa na mtu au taasisi”.**

9. Kanuni ya 4(2), inarekebishwa kwa kufuta maneno **“taasisi au jumuiya itaruhusiwa”** na kuweka badala yake maneno **“muombaji ataruhusiwa”.**

10. Kanuni ya 4(3) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“taasisi au jumuiya itakayoanzisha”** kuweka badala yake maneno **“muombaji atakaeanzisha”** yaliopo mwanzoni mwa Kanuni hiyo.

11. Kanuni ya 4(4)(b) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“mtu binafsi”** na kuweka badala yake neno **“muombaji”** mwishoni mwa Kanuni hii.

12. Kanuni ya 4(4)(c) inarekebishwa kwa kufutwa maneno **“nyaraka za usajili wa taasisi au jumuiya;na”** na kuweka badala yake maneno “**nyaraka za usajili wa taasisi au vitambulisho vya mtu binafsi**”.

13. Aidha, Kanuni ya 4(4)(d) inaonekana kuwa haipo sawa kwa sababu Kanuni inazungumzia **maombi ya usajili na viambatanisho** vyake hivyo ni vyema vikaainishwa wazi

14. Kanuni ya 4(5) inarekebishwa kwa kuongeza “**endapo zitapita siku kumi na nne bila ya ombi la muombaji kujibiwa au kupewa taarifa yoyote iiliyorasmi itachukuliwa kuwa maombi hayo yamekubaliwa”.**

15. **Kuandikwa Kanuni mpya ya 7 ambayo itazungumzia mambo yafuatayo:**

1. **waziri atashughulikia rufaa ndani ya siku kumi na nne tokea tarehe ya kuwasilishwa rufaa hiyo,**
2. **katika kushughulikia rufaa waziri anaweza;**
   - i. **kukubaliana na maamuzi ya Mkurugenzi au kukataa pamoja na kuainisha sababu,**
   - ii. **kutoa maelezo kwa Mkurugenzi au**
   - iii. **kumtaka Mkurugenzi alizingatie tena ombi husika.**

16. Kanuni ya 7 kuwa Kanuni ya 8 na Kanuni zinazofuata zifuate mpangilio wa wake.

Kanuni ya 7 ambayo kwa sasa ni Kanuni ya 8 inarekebishwa kama ifuatavyo;

- Aya ya (a) kufuta na kuandika upya kama ifuatavyo" **"jina la muombaji anayeanzisha makaazi".**

- Aya ya (f) Mkurugenzi inatakiwa aziweke wazi Taarifa zote zinazotakiwa ndani ya kanuni hizi.aidha, Kamati inashauri kuandwa kama ifuatavyo: **"taarifa nyengine ambazo Mkurugenzi ataona zinafaa kwa maslahi bora ya wazee".**

Kanuni ya 7(3) kamati inashauri kufutwa na kuandikwa umpya kama ifuatavyo:

7(3) (a) **"daftari la kumbukumbu la usajili litakuwa chini ya usimamizi wa Mkurugenzi**".

(b) "**Mkurugenzi anaweza kukasimu madaraka ya usimamizi wa daftari la kumbukumbu kwa Afisa wa ustawi wa jamii yeyote anayeona anafaa."**

Kanuni ya 7(4) Kwa kufuta neno "**aliyeteuliwa"** na kuweka badala yake neno **"aliyekasimiwa"** liliopo mwanzoni mwa mstari wa pili wa kanuni 7(4)

Kanuni ya 7(5) inarekebishwa kwa kufuta neno **"muda"** liliopo baina ya neno **"ya"** na **"kama**" na kuweka badala yake maneno **"mwaka au wakati wowote Mkurugenzi atapoona kama kuna haja ya kufanya hivyo"**

17. Kanuni ya 8, Kamati ishauri katika wajumbe wa Kamati ya tathmini Mkurugenzi atoke kwa sababu Kamati hiyo ikimaliza kazi yake ripoti inawasilishwa kwake au vyenginevyo ripoti hiyo isiwasilishwe kwa Mkurugenzi.

Pia Kamati inashauri uwepo wa Katibu ambaye atakuwa **Afisa ustawi wa jamii,** kwa ajili kuandaa ajenda za kazi, kuweka kumbukumbu na kuandaa ripoti.

Aya ya 8(b) Kamati inashauri itoke.

Kamati inashauri kuwekwa **Afisa Ustawi Jamii muandamizi kuwa mwenyekiti wa kamati hii.**

Kamati inashauri kuwekwa Suala la muda kukutana kamati hiyo.

Kanuni ya 9(2)(d) kuongeza neno mavazi baina ya neno “chakula” na “malazi”.

Kanuni ya 9(2) (e) kuongeza maneno “**kwa ustawi bora wa wazee”** mwishoni mwa aya hiyo.

18. Kanuni ya 10 kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo: “**Mkurugenzi anaweza kusimamisha makaazi kutoa huduma muda wowote endapo ikionekana kwamba mtoa huduma amekwenda kinyume na masharti yaliowekwa ndani ya Kanuni hizi”**.

Kanuni ya 10(3) inarekebishwa kwa kifutwa maneno “**isipokuwa kamaitaelekezwa vyenginevyo”** na kuweka badala yake maneno “**hadi pale ambapo masharti ya kutoa huduma yametimizwa”**.

19. Kanuni ya 11 kufuta maneno “**mtu ambaye**” yaliopo mwanzoni mwa kanuni hiyo na kuweka badala yake neno **“Muombaji”.**

Kanuni ya 11(1)(a) inarekebishwa kwa kufuta na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo; **“kivuli halisi cha kitambulisho cha mzanzibar mkaazi**, **mtanzania au hati ya kusafiria endapo muombaji ni mtu binafsi”**.

20. Kanuni ya 12 (1) inarekebishwa kwa kuingiza maneno "**kupitia ripoti ya tathmini na"** baina ya neno **"ya**" na "**kuridhika"**

21. Kanuni ya 14 inarekebishwa kwa kuingiza maneno **"inaweza kuhuishwa"** baina ya neno **"hizi"** na **"kila"**

Kanuni ya 12 (1) inarekebishwa katika maneno ya Pembeni kwa kufuta maneno "**wajibu wa taasisi au jumuiya**" na kuweka badala yake maneno "**wajibu wa muombaji**".

22. kanuni 18(1)(g) kamati inashauri mzee akingia katika makaazi ndipo afanyiwe uchuguzi wa afya.

23. Kanuni 20(2) inarekebishwa kwa kufuta maneno ya mwisho "**mzee husika anayetaka kuingia katika makaazi kama ametimiza masharti na vigezo chini ya kanuni hizi**" na kuweka badala yake maneno "**kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 18 ya Kanuni hizi ili kuangalia kama mzee anayetaka kuingia katika makaazi kama ametimiza masharti na vigezo chini ya Kanuni hizi".**

24. Kanuni ya 22 inarekebishwa kama ifuatavyo:

1. **Kutakuwa na daftari la wageni katika makaazi yote ya wazee.**
2. **Kila mgeni anayetembelea makaazi ya wazee atalazimika kuandika taarifa zake katika daftari la wageni kama itakavyoainishwa katika daftari hilo.**
3. **daftari la wageni litajumuisha taarifa zifuatazo**:

katika kanuni ya 23na 24 neno **"afisa ustawi wa jamii", "afisa ustawi wa jamii wa wilaya" "afisa dhamana" na "afisa makaazi"** kamati inataka kufahamu ni ipi tofauti yao.

Kanuni ya 24(2) inarekebishwa kwa kufuta neno "**masaa"** na kuweka badala yake neno "**saa".**

Kanuni ya 22 inarekebishwa kwa kufuta maneno ya pembeni "**utaratibu wa kupokea wageni**" na kuweka badala yake maneno **"daftari la wageni**".

25. Kanuni ya 26 (1) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"miezi mitatu"** na kuingiza maneno **"katika miezi mitatu mara moja"** baina ya neno **"angalau"** na **"miezi".**

26. Kanuni ya 29 inarekebishwa kwa kufuta maneno ya pembeni "**makosa yanayofanywa na taasisi au jumuiya"** na kuweka badala yake maneno **"makosa yanayofanywa na muombaji".**

Aidha, inarekebishwa kwa kufuta maneno **"taasisi au jumuiya"** na kuweka badala yake neno **"muombaji".** Pia katika aya (a), (b), (c), (d) na (d) kufuta maneno **"itafungua, itatoa, itamruhusu, itaendelea na itaendesha"** na kuweka badala yake maneno yafuatayo **"atafungua, atatoa, atamruhusu, ataendelea na ataendesha".**

27. **Kanuni ya 32 inarekebishwa kwa kufuta maneno "taasisi au jumuiya"** na kuweka badala yake maneno **"muombaji".**

**Naomba kuwasilisha**

**.........................................**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

**KIAMBATANISHO NAMBARI 5**

**AMRI YA VIWANGO VYA MWENDO VYA KIMATAIFA KWA BARABARA ZOTE ZA ZANZIBAR**

Kamati baada ya kupitia AMRI hii kwa kina pamoja na kukutana na wadau mbali mbali, ilibaini kasoro katika Amri hii na changamoto mbali mbali miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na: Kukosekana kwa uelewa kwa baadhi ya wadau juu ya uwepo wa Amri ya viwango vya mwendo vya kitaifa kwa barabara zote.

- ✓ Kukosekana kwa ufafanuzi wa baadhi ya maneno ambayo ni muhimu kuwepo ndani ya amri hii.
- ✓ Amri imejikita kiwango cha juu cha mwendo kwa maeneo ya mjini na vijijini katika jaduweli lake, hoja iliyojitokeza ni kwamba maeneo ya biashara na hatarishi yameangaliwaje hasa katika viwango kilichowekwa kwa upande wa vijijini.
- ✓ Aidha suala la kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari juu ya uwepo wa Amri hii ya viwango vya juu vya mwendo kwa maeneo ya mjini na vijiji ni muhimu sana
- ✓ Suala la vyombo ambavyo havisajiliwi utaratibu wake umewekwa wapi na utakuwaje.

Mbali na hayo Kamati ilipata fursa ya kupitia Amri ya Viwango vya Mwendo vya Kimataifa kwa Barabara zote za Zanzibar hiyo na kubaini mambo yafuatayo:

Katika Amri ya 2, ya ufafanuzi wa maneno kamati inashauri kufanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:

a) **Neno "chombo cha moto"** linarekebishwa kwa kuingiza maneno **"kinavyotumia chagi na"** baina ya neno "**chombo"** na **"kinachokwenda".**

b) **Neno "dereva" Aya ya (a)** linarekebishwa kwa kufuta maneno **"maana yake ni mtu anayendesha au anayejaribu kuendesha au mwenye dhamana ya chombo cha moto hicho na inajumuisha mwalimu wa dereva mwanafunzi; au".**

   Aya ya (b) inarekebishwa kwa kufuta neno **"inayovutwa"** na kuwekwa badala yake neno **"inayovuta" liliopo mwishoni mwa amri hiyo.**

Kamati inashauri kuwekwa tafsiri ya neno "**adhabu ya papo kwa papo"** kwa mujibu wa amri hii.

Amri ya 3(1) inarekebishwa kwa kufuta na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo;

**"kutakuwa na kiwango cha njuu cha mwendo kwa maeneo ya mjini na vijijini ya barabara zote za Zanzibar kama vilivyoelezewa katika jadweli la kwanza la Amri hizi."**

Amri ya 3(2) inarekebishwa kwa kufuta maneno "**na aina ya vyombo vya moto vilivyoendeshwa"** na kuweka badala yake maneno **"husika"**

Kamati inashauri amri ya 4(1) kiwango cha juu cha mwendo kiangaliwe kilingane na kiwango kilichowekwa katika Sheria.

Amri ya 4(1) inarekebishwa kwa kufuta nano **"ni"** liliopo baina ya neno **"mwendo"** na **"kilomita"** na kuweka badala yake neno **"kisichozidi"**

Amri ya 6(1) inarekebishwa kwa kufuta maneno "**itampa taarifa ya maandishi"** yaliopo baina ya neno **"Mamlaka"** na "**dereva"** na kuweka badala yake maneno "**itampatia fomu ya utaratibu wa kumalizia kosa"**

Kamati inashauri kufutwa Kanuni 6 (2) kwani maelezo yake yanajitosheleza katika jaduweli wa pili ya amri hizi.

Aidha, endapo Mamlaka itaona kwamba kuna haja ya kuongeza maelezo mengine yoyote muhimu yanahitajika kuwepo yaingizwa katika jaduweli husika.

a) Amri ya 6(3) inafutwa na kuandikwa upya na kwa sasa itakuwa Amri ya 6(2) na itasomeka kama ifuatavyo;

"**dereva atakayepewa fomu ya utaratibu wa kumaliza kosa chini ya Amri ndogo ya (1) ya Amri hii atatakiwa kulipa faini kwa Mamlaka kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa katika Amri ya 5 ya Amri hizi. Ndani ya siku saba kutoka siku aliyokamatwa.**

b) Amri ya 6(4) inafutwa na kuandikwa upya na kwa sasa itakuwa Amri ya 6(3) na itasomeka kama ifuatavyo;

**“endapo dereva atashindwa kutekeleza masharti chini ya amri ndogo ya (2). Mamlaka itachukua hatua nyengine za kisheria dhidi ya dereva huyo”.**

Amri ya 6(5) inafutwa na kuandikwa upya na kwa sasa itakuwa Amri ya 6(4) na itasomeka kama ifuatavyo;

**Bila ya kujali Amri ndogo ya (3) ya Amri hii, endapo dereva atalipa faini iliyoainishwa katika Amri ya 5(1) ya Amri hizi ambacho kimeainishwa katika fomu ya kumaliza kosa, hakuna hatua za kisheria zitakazochukuliwa kuhusiana na kosa hilo kwa dereva huyo”.**

Kamati inashauri Amri ya 7 kufutwa kwani Amri au Kanuni haiwezi kufuta Sheria yoyote.

**JADWELI LA PILI:**

Kamati inashauri aina ya faini ziwekwe kwa kosa la mwanzo na pili. Aidha, namba ya chombo kilichokamatwa kiainishwe.

**Naomba kuwasilisha**

**.............................................**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

## KIAMBATANISHO NAMBARI 6

## MAJUMUISHO YA KANUNI ZA THAMANI YA FIDIA ZA MAZAO NA MITI

Kamati baada ya kupitia Kanuni za Thamani ya Fidia za Mazao na Miti pamoja na kukutana na Wadau ilibaini kasoro kadhaa katika

Kanuni hii na changamoto kadhaa. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:

Kamati imebaini kwamba Wadau waliokutana nao wengi wao sio ambao walishiriki katika utungwaji wa Kanuni hizi. Kamati inashauri wakati wa kuwaita wadau kutoka katika Taasisi mbali mbali kwa ajili ya kutoa maoni yao kuhakikisha wadau hao kuwa wajumbe kwa wenzao ili endapo wakati Kamati inataka maoni kutoka kwa Wadau isiwe kama kila mmoja wao haelewi kanuni husika.

Kamati imebaini kukosekana kwa ufafanuzi wa baadhi ya maneno ambayo ni muhimu kuwepo ndani ya Kanuni hii.
Mfano neno eka, ekari, shina, koongo na tuta.
Aidha, Kamati inashauri kutumia maneno kwa kufuta nidhamu ya uandishi kama maneno mawili yenye maana moja kutumika katika andiko moja sio sahihi kanuni hii imetumia neno eka na ekari yakiwa na maana moja.
Kamati inashauri kuwekwa kwa ufafanuzi wa maneno ambayo yatasaidi kuifanya Kanuni hii inasomeka vizuri zaidi na kuweza kufahamika kwa urahisi.

Pia, Kamati inataka ufafanuzi katika jadweli kwamba kuna baadhi ya mazao yanaonekana yameekewa daraja zao lakini kuna nyengine hayakuwekewa.

Vilevile, Kamati, inashauri kuwa madhumuni ya kanuni hii yaende sambamba na yaliomo ndani kanuni inakusudia kulipa fidia za miti na mazao kwa kawaida kinachopewa thamani ni mti na sio tunda linalotokana na mti kwani kamati imebaini baadhi ya vichwa vya habari vinazungumzia matunda badala ya miti mfano;

- mazao jamii ya ndimu ilipaswa kuwa miti ya jamii ya ndimu,
- matunda ilipaswa kuwa ni miti ya matunda,n.k.

Kamati imebaini pia Kanuni imekosa kuwa na kanuni inayoonesha Mawanda ya matumizi Kanuni hizi hivyo inashauri iwekwe kanuni inayoonesha mawanda yake.

Kamati inashauri katika Kanuni ya 3 inarekebishwe kwa kufuta neno **“zinafutwa”** na kuweka badala yake **“zinaondolewa”.** Kwani sheria ndogo ikijumuisha kanuni huwa zinaondolewe (**revoked**) na sio kufutwa (**repealed**) kwa mujibu wa uandishi wa Sheria.

Kamati inashauri kuangaliwa tena Zao la Miwa liliomo ndani ya jadweli, kuthamanishwa kwa tuta ambapo haioneshi uhalisia wake.

Kamati inashauri kuangaliwe upya kwa bei za baadhi ya mazao kulingana na hali halisi ya soko na gharama za kuandaa shamba mpaka kupatikana kwa mazao hayo miongoni mwa mazao ambayo ilishauriwa kuangaliwa upya thamani za fidia kama yafuatayo; fiwi, vanilla, hiliki, mbatata, miti kama mianzi na mengineyo.

Pia, kuangalia bei ya aina ya migomba baina ya mtwike na jamii ya mzuzu.

**Ushauri wa jumla**

Kamati inashauri utaratibu wa ulipaji wa fidia usiwe unachukuwa muda mrefu baada ya kufanywa kwa tathmini. Aidha, miongozo ya ulipaji wa fidia iandaliwe ili iweze kutumika na kurahisisha uwelewa kwa masuala ya fidia kwa wahusika.

Aidha, Kamati inashauri suala la fidia ya haki ya ardhi nalo lizingatiwe.

**Naomba kuwasilisha**

**…………………………………………**

**MWENYEKITI KAMATI YA KANUNI**

**SHERIA NDOGO NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**<u>ZANZIBAR</u>**

**<u>KIAMBATANISHO NAMBARI 7</u>**

**<u>MAPENDEKEZO MAHSUSI YA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR FAO LA KUUMIA KAZINI</u>**

28. Kanuni ya 1, inarekebishwa kwa kufuta neno **“Mheshimiwa”**.

29. Kanuni ya 2, inarekebishwa kwa kufuta maneno “**Zanzibar”** kwa sababu kanuni hii inatokana na Sheria inayotumika Zanzibar, hivyo hakuna haja kusema kanuni hizi itatumika wapi**.**

30. Kanuni 2(3), inarekebishwa kwa kufutwa na kuunganishwa na kanuni ya 1, kwani ni kanuni inayozungumzia kuanza kutumika kwa kanuni hizi ambayo hiyo ni kanuni ya 1, (commencement) kwa mujibu wa utaratibu wa uandishi (the Law of interpretation).

Hivyo kanuni ya 1 inarekebishwa kwa kuongeza kanuni ndogo ya (2) na itasomeka kama ifuatavyo: **“bila ya kuathiri kanuni ndongo (1) ya kanuni hii malipo ya fao la kuumua kazini yataaza kulipwa kwa wafanyakazi kuanzia tarehe 1 Julai 2023”.**

Aidha, marekebisho hayo yatapelekea kanuni ya 1, kuwa “1-(1) …….”

31. Kamati inataka kufahamu kwamba kanuni ya 2, imeainisha wafanyakazi wanaopaswa kulipwa Fao la Kuumia kazini ni wanachama wote wa mfuko lakini kanuni ya 2(4) inaeleza kuwa Waziri anaweza kujumuisha wafanyakazi wengine kupata mafao ya kuumia kazini;

I. Jee wafanyakazi hao wanatoka wapi?
II. Jee wasiokuwa wanachama wanaweza kufaidika na Fao hilo au ni nini madhumuni ya kanuni hiyo?

32. Kanuni ya 6(c) ambayo inaeleza matumizi ya fedha za Skimu ya Fidia kuwa miongoni mwa matumizi yake zitatumika kuimarisha uwepo wa usalama na afya kazini. Mfuko umeona kanuni hii inaweza kuleta changamoto hasa ikizingatiwa kuwa jukumu la kuimarisha usalama na afya kazini ni jukumu la Idara ya Usalama na Afya Kazini ambayo iko chini ya Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji. Hivyo, Mfuko unapendekeza kanuni ya 6(c) ifutwe ili kuepusha kujitokeza changamoto hiyo. Kanuni ya 8(b) inarekebishwa

kwa kufutwa maneno **“au ripoti”** kwa sababu yana maana moja.

Kanuni ya 10(3) Kamati inashauri kuwekwe muda maalum ambao mfanyakazi atakuwa amelipwa mafao mara baada ya kuumia.

33. Kanuni ya 11(4) itambue mshahara au pato la mwezi ambalo mfanyakazi alikuwa anapata kabla hajaondoka kazini badala ya kusema kuwa pato la mfanyakazi litaamuliwa na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar.

34. Kanuni zinazohusiana na ukokotoaji wa mafao ya kuumia kazini ikiwemo kanuni ya 13(2) na 15(2). Kanuni hizi zinaweza kuleta changamoto inayoweza kupelekea Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar kulipa kwa kiwango kikubwa hasa kutokana na sababu kwamba kanuni hizi zinaelekeza kutumia pato la mwezi la mfanyakazi(mshahara) ikizingatiwa kuwa wako wafanyakazi au wanachama wa Mfuko ambao wanafikia kulipwa mshahara wa mwezi wa takriban milioni 30 hasa wafanyakazi kutoka sekta binafsi. Katika kuepusha kutokea changamoto hiyo Mfuko unapendekeza yafuatayo:-

i. Kanuni itambue na iweke mazingira ya ukokotoaji wa fao la kuumia kazini kutumia ukomo wa mshahara (earning ceiling) ulioainishwa katika Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Na.2 ya mwaka 2005 ambao si zaidi ya TZS 7,500,000 tu.

ii. Kanuni iweke na itambue uwepo wa kima cha chini na kima cha juu cha malipo ya fao la kuumia kazini ikiwa viwango maalum vya fedha zitakazolipwa.

35. Utaratibu wa malipo ya mafao yanayolipwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar kwasasa hauruhusu mwanachama kulipwa mafao mawili (2) au zaidi ya moja kwa wakati mmoja na ikitokea mwanachama anastahili kulipwa mafao zaidi ya moja analipwa fao moja ambalo ni kubwa zaidi. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar kwasasa unapendekeza kanuni hii iruhusu mwanachama kulipwa mafao zaidi ya moja kwa wakati mmoja hasa iwapo itatokea mwanachama amefariki kutokana ajali kazini alipwe fao la urithi la kawaida na fao la kifo kilichotokana na ajali au maradhi akiwa kazini. Aidha, mwanachama ambae amepata ulemavu wa kudumu unaotokana na kazi alipwe fao la ulemavu la kawaida (invalidity benefit) na fao la ulemavu kutokana na ajali kazini.

36. Kanuni ya 15(2) irekebishwe kwa kukokotoa fao la kifo kwa miezi 36 badala ya miezi 48 iliyopo sasa ili kwenda sambamba kama ilivyo katika Sheria.

37. Kanuni ya 26, Kamati inashauri jukumu hili liondolewe kwa mwajiri kwani muajiri amechangia mafao hayo kwa mfuko kwa kila mfanyakazi wake.

38. Kanuni ya 29(1) inarekebishwa kwa kuingiza maneno “**za kazi”** baada ya neno **“saba”.**

39. Kanuni ya 32(2) Kamati inashauri kuzingatiwa siku badala ya **“siku kumi na nn**e” kuwa **“siku thelathini’’**.

40. Kanuni ya 34, kamati inataka kufahamu kuhusu wafanyakazi wa sekta binafsi ambao wengi wao wanatumia bima katika hospitali za binafsi.
Je hakutakuwa na kutokutekelezeka kwa masharti ya kanuni hii.

Kamati imefanya mapitio ya jadweli la kwanza hadi la tatu ya kanuni hizi na imebaini changamoto nyingi zinazohitaji kufanyiwa kazi hasa ukizingatia baadhi ya taarifa zinatofautiana na uhalisia wa athari zenyewe hivyo Kamati inashauri

41. Kanuni ya 41 itenganishe makosa ya aina tofauti na adhabu zake kwa kuwa baadhi ya makosa na adhabu zilizowekwa hayaendi sambamba na kurekebisha viwango vya kutoza faini kwa kuweka faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano (5) badala ya Shilingi Milioni Moja (1).

42. Kanuni ya 43(1) ifutwe kwani kilichoelezwa na kanuni hii ni jukumu la kawaida la Idara ya Usalama na Afya Kazini Zanzibar na hakuna umuhimu wa kuainishwa katika kanuni hizo.

43. Kanuni iweke sharti kwa waajiri kuwa na cheti cha OSH kwa upande wa waajiri wa Zanzibar na cheti kutoka OSHA kwa waajiri wa Tanzania Bara ambao wanachangia ZSSF.

44. Kanuni ya Fao la Kuumia Kazini 2023 impe Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar uwezo wa kutayarisha na kutoa Miongozo ya aina tofauti ikiwemo miongozo inayohusiana na Tathmini ya Ulemavu au Maradhi (Assessment of Impairment and Assessment of Disability).

**Naomba kuwasilisha**

..........................................

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

**KIAMBATANISHO NAMBARI 8**

## MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KATIKA KUPITIA KANUNI YA (FAO LA UPOTEVU WA AJIRA)

1) Kanuni hii inatokana na Sheria namba 2 ya mwaka 2005, kufuatia marekebisho ya Sheria hiyo ya 2021, ili iweze kukidhi haja ya mabadiliko ya kiichumi na ya kijamii yanayotokea.

2) Kamati imefanya mapitio na inashauri yafuatayo:

3) Kanuni ya 2 neno **"mkurugenzi mwendeshaji"** linarekebishwa kwa kufuta maneno **"chini ya"** yaliopo mwishoni mwa mstari wa pili wa neno hilo.

4) Kanuni ya 3(4) Kamati inataka kupata ufafanuzi kwa nini isiwe kwa ridhaa ya mwanachama kupeleka michango kwenye mfuko wa hiyari.

5) Kanuni ya 4(2) inarekebishwa kwa kufuta neno **"mwananachama"** na kuweka badala yake neno **"mwanachama"**

6) Aidha, Aya ya (d) inazungumzia kuhusu kuambatanisha Mkataba wa Ajira katika fomu ya maombi ya Mafao ya Upotevu wa Ajira kutoka kwa mwanachama wakati huo huo muajiri nae anatakiwa kuwasilisha Mtakaba wa Ajira kwa mujibu wa Kanuni ya 9. Je, kuna ulazima gani kwa mwanachama kuwasilisha katika viambatanisho anavyotakiwa kuambatanisha pamoja fomu ya maombi hayo ambapo nyaraka hizo tayari taasisi inazo?

7) Kamati inataka kufahamu kwamba kuna uhusiano gani wa kutoa "taarifa za hesabu yake ya benki" katika suala la viambatanisho baada ya kujaza fomu ya maombi maalumu ya upotevu wa ajira.

8) Aya ya (f) Kamati inahitaji maelezo kama kuna umuhimu wa kuweka aya hiyo ambayo ipo na utata (mkanganyiko)

9) Kanuni ya 5 Kamati inataka kuelewa busara ya kutumia miezi 24 kwa mwanachama anayetaka kupata fao kwa mara ya pili na isiwe muda wa miezi 18 kama awali anayepewa fursa hiyo.

10) Kanuni ya 6 utaratibu wa utoaji wa mafao umewekwa katika njia tatu tofauti je, katika kuamua hivyo ushiriki wa wadau ulizingatiwa kwani wao ndio wanao wawakilisha wanufaika wa utaratibu huo.

11) Kanuni ya 7 Kamati inashauri kuwekwa bayana maneno "kipindi Fulani" yaliojitokeza katika Kanuni hiyo ambayo hayana tafsiri moja hivyo yanaweza kuleta utata.

12) Katika fomu ya maombi ya "**fao la upotevu"** wa ajira (Kipengele cha 2) fomu yenyewe inazungumzia **"ukosefu wa ajira"** wakati Kanuni yote ni upotevu wa ajira. Kamati inahitaji uwiano wa matumizi ya maneno.

13) Vile vile, yapo makosa ya kiuandishi katika fomu nayo yawekwe sawa

14) Kipengele cha 4 maneno **"Afisi ya Kuu"** yawe **"OfisiKuu"**

**NAOMBA KUWASILISHA**

………………………………
**Mihayo Juma N'hunga**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar**

**KIAMBATANISHO NAMBARI 9**

**KANUNI ZA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA 2023, KWA AJILI YA MAMLAKA YA KUDHIBITINA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA – ZANZIBAR**

Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya Zanzibar, imeunda Kanuni za kudhibiti na kupambana na dawa kulevya 2023, kupitia Sheria yake nambari 8 ya mwaka 2021, kwa ajili ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar.

Kamati imebaini kuwa Kanuni hiyo ina changamoto ya muingiliano wa majukumu ya kazi na Sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar, Sheria nambari 10 ya mwaka 2011, na Kanuni za Kemikali za Viwandani na Majumbani za Mwaka 2014.

Miongoni mwa changamoto hizo zimejitokeza katika Kanuni ya 19 hadi 29 ni:
Kamati inashauri Kanuni ya 19 hadi 29 zifutwe kwa sababu:

1. Kanuni hizi zimechukuliwa kutoka kwenye Kanuni ya Kemikali za Viwandani na Majumbani,

2. Kuepuka muingiliano wa Sheria na Kanuni kwa upande wa majukumu ya kiutendaji lakini pia kuepuka usumbufu kwa wananchi watakaohitaji kutumia kemikali,

3. Mkemia Mkuu ndio mwenye Mamlaka na jukumu pekee la kusimamia Kemikali na sio Taasisi nyengine yoyote kwa mujibu wa Sheria Nambari 10 ya mwaka 2011. Aidha, kupitia Kanuni yake ya mwaka 2014, imeweka utaratibu wote kuhusu Kemikali namna ya kuhifadhi, kusafirisha, uingizaji na utoaji ambapo hakuna eneo lilinalozungumzia kushauriana na Taasisi nyengine yoyote hiyo Kamati inashauri kuangaliwa tena suala hilo kwani ni mgongano wa majukumu kisheria. Aidha, inashauri Mamlaka kukaa pamoja na Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar na kujadili suala hili ili kuhakikisha majukumu haya hayagongani kisheria.

4. Sheria ya Wakala kupitia Kanuni ya mwaka 2014 ya Kemikali za Viwadani na Majumbani imelezea kuhusiana na Kemikali Bashirifu katika Kanuni ya 29 na kutaja orodha ya Kemikali Bashirifu katika jadweli la 9 na baadhi ya Kanuni nyengine zimelezea namna ya udhibiti wa Kemikali ni Mkemia Mkuu, hivyo ni suala la busara kukaa kikao na Mkemia Mkuu ili kutafuta uhalali kwa mujibu wa Sheria.

5. Kamati inashauri katika Kanuni ya 4, ifanyiwe marekebisho kama ifuatavyo;
    i. Kuongezwa maneno yanayoonesha dhana ya kutaifisha Kemikali Bashirifu zilizokamatwa kutumika katika Taasisi nyengine kama Taasisi zinazotumika kemikali na shule n.k.

    ii. Mwakilishi kutoka ZEMA iwe miongoni wa wajumbe watakaohudhuria katika uteketezaji wa dawa hizo, kwani Kamati imebaini katika Kanuni ya 4(1) kuwepo kwa upungufu wa kutozingatiwa Mjumbe muhimu kutoka

Mamlaka ya Mazingira (ZEMA) ambae yeye ndo mtaalamu atakaeweza kutoa tathmini ya eneo husika pamoja na mazingira halisi na athari zitakazoweza kujitokeza na hatua za kuchukuliwa baada ya kujitokeza athari hizo.

**iii.** Kamati inapendekeza Mkemia Mkuu asiwe peke yake awekwe **au Mwakilishi wake.**

iv. Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto katika Kanuni ya 4(2) inayozungumzia utekezaji wa dawa za Nakotiki, Saikotropiki na Kemikali Bashirifu ambapo katika Kanuni ndogo hiyo ya (2) Mamlaka imejipa uwezo panapokuwa na dharura baada ya kupata idhini ya Mahakama kuziteketeza dawa hizo bila kuwepo kwa wahusika waliotajwa katika Kanuni ndogo ya(1) ambapo jambo hilo ni kinyume na utaratibu wa kisheria kwani jambo hilo haliwezi kutekelezeka hadi Mkemia Mkuu au Mwakilishi wake kuwepo kwenye uteketezaji huo. Kamati imeliona hilo kama ni mgomgano wa kimajukumu baina ya Taasisi mbili kati ya Mamlaka ya Madawa ya Kulevya Zanzibar na Ofisi ya Mkemia Mkuu Zanzibar.

6. Kanuni ya 10(2) inarekebishwa kwa kuongeza aya mpya (e) na kusomeka kama ifuatavyo;
**"Mamlaka zilipokamatwa dawa kama kifungashio, bahasha, mkoba au begi."**

7. Kanuni ya 11 inarekebishwa katika mwaka wa Sheria kwa futwa "2001" na kuweka badala yake "2011". Aidha, kamati inashauri kila eneo yaliopojitokeza hayo yawekwe sawa.

8. Kanuni ya 12 inarekebishwa kwa kufutwa maneno **"afisa aliyeidhinishwa ambaye amepewa idhini ya maandishi"** na kuweka badala yake maneno **kamishna mkuu au a……….".**

9. Kanuni ya 17(1)(g) kifanyiwe marekebisho kwa sababu mwenye jukumu la kufanya usajili wa Kemikali Bashirifu ni Mkemia tu. Aidha, Mkemia Mkuu ndio mwenye Mamlaka yote ya Kudhibiti Kemikali kwa mujibu wa Sheria nambari 10 ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2014.

Hivyo kuanzia Kanuni ya 19 hadi 29 na nyengine zinazomtaka Mkemia Mkuu kushauriana na Mamlaka zifutwe kwani kufanya hivyo ni kujipa ukuu juu ya Sheria nyengine (Overriding power of other laws) hivyo basi kamati inataka kujua mmoja tu mwenye jukumu hilo. Kwani kuwacha hivyo kutapelekea muingiliano wa kimajukumu baina ya Taasisi mbili na kupelekea ucheleweshaji wa muda wa wateja.

Aidha, Kanuni ya 23(1) (a-i) - 23(2) ninayozungumzia kazi za Maabara ya Sayansi Jinai. Ambapo uudwaji wa Kanuni hizo umefanywa kwa kutumia kifungu cha 84(1) na 84(2)(c) cha Sheria nambari 8 ya mwaka 2021 ya kuanzishwa Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya Zanzibar, ambapo kifungu hicho hakijamlazimisha Waziri kimempa hiari tu ya kuweza kutunga Kanuni ya uchukuaji wa Sampuli na upimaji pamoja na uchambuzi wa Sampuli hizo. Wakati Sheria ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali nambari 10 ya mwaka 2011, ambapo kifungu 5(1), (2), (3) na (4) (a-j) kimeeleza kuwa Maabara ndio itakua ni Chombo kikuu cha ushauri cha Serikali, kwa mambo yanayohusiana na Sayansi jinai, uchunguzi wa Maabara juu ya chakula, dawa, dawa ya kulevya, usimamizi wa kemikali na sumu. Kwa kuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imepewa uwezo kisheria wa kudhibiti wa kemikali kupitia Sheria nambari 10 ya 2011 na Kanuni za Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani za 2014, hivyo kufuatia utungwaji wa Kanuni mpya za Mamlaka za kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya za 2022. Kamati imeona kwamba kutakuwa na changamoto ya kuingiliana

majukumu katika eneo la Kusimamia na Kudhibiti Kemikali Bashirifu.
Kanuni hizo zina changamoto ya muingiliano mkubwa wa majukumu ya kazi na Sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar, Sheria nambari 10 ya mwaka 2011, na Kanuni za Kemikali za viwandani na majumbani za mwaka 2014. Miongoni mwa changamoto hizo zimejitokeza katika Kanuni ya 7 hadi 29 ambapo zimeonekana kugongana kimajukumu na Kanuni za Kemikali za viwandani na majumbani za mwaka 2014, zinazotokana na Sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar.

Kwa ujumla, Kamati imeweza kuainisha baadhi ya changamoto hizo, na imeona ni vyema na ni busara kwa kuzingatia mipaka ya Sheria ni vyema wahusika hao Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kukaa pamoja na kuweza kuzipatia utatuzi na kuziondosha changamoto zote hizo za kisheria.

Hivyo, Kamati inashauri Mamlaka hizo kuandaa kikao cha pamoja kuziainisha changamoto zilizomo ndani ya Kanuni hizo na kuzipatia uamuzi kisheria ili Kanuni hizi ziwe ndani ya mipaka na zisije kugongana na Kanuni za Sheria nyengine kiutekelezaji. Aidha, Kamati inatarajia kuona **Ripoti ya Mapendekezo ya Kikao** hicho kwa ajili ya kuendelea na taratibu zake za kuridhia matumizi ya Kanuni hizo.

**KIAMBATANISHO NAMBARI 10**

## MAJUMUISHO KANUNI ZA UTUMISHI ZA MAMLAKA YA UTHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR, 2013

Kamati baada ya kupitia Kanuni hizi na kusikiliza maoni ya Wadau ilibaini kasoro na changamoto kadhaa ambazo zinahitaji kurekebishwa ili kanuni hiyo iweze kufikia malengo yaliyokusudiwa Mamlaka.

Miongoni mwa changamoto za Watumishi wa Mamlaka hio ni pamoja na:

- ✓ Kukosekana kwa uelewa kwa baadhi ya watendaji wa Mamlaka juu ya uwepo wa Kanuni ya Utumishi ya Mamlaka.
- ✓ Kukosekana kwa posho la mazingira magumu
- ✓ Posho la sare haliendani na mahitaji yao kwa mwaka.
- ✓ Kuondoshwa kwa posho la siku za Ramadhani na Sikukuu.
- ✓ Likizo ya huruma ihusishe na mkwe.
- ✓ Posho la uzazi lizingatie na baba wa mtoto.

- ✓ Kuzingatiwa kwa watu wenye mahitaji maalum wakati wote haswa katika kipindi cha muda wa majaribio.
- ✓ Likizo kipindi cha ndoa iongezwe kufikia wiki mbili. Wiki moja iwe kabla na wiki moja baada ya ndoa.
- ✓ Elimu kwa wafanyakazi juu ya Kanuni hizi itolewe kila baada ya kipindi fulani.
- ✓ Elimu kwa wafanyakazi wanaoelekea kustaafu itambuliwe na Kanuni hizi.
- ✓ Mafunzo ya watumishi katika muda wa majaribio yatambuliwe na Kanuni.
- ✓ Posho la kutunza siri lizingatiwe ndani ya Kanuni.

Mbali na hayo Kamati ilipata fursa ya kupitia Kanuni hiyo na kubaini mambo yafuatayo:

1. Kamati inahitaji ufafanuzi wa Kanuni ya 4, kuhusu **Mkurugenzi Mkuu** au **Naibu Mkurugezi Mkuu** kiuandishi inatakiwa kuandikwa kama ifuatavyo;

“a) **Mkurugenzi Mkuu atakuwa mwenyekiti na endapo atakuwa hayupo Naibu Mkurugenzi Mkuu atakaimu nafasi hiyo”.**

Aidha, nibusara Mkurugenzi Mkuu kwa kushirikiana na Mkurugenzi Rasilimali watu watamchagua Mkuu wa Sekritariati na wenzake watakaomsaidia badala ya Mkurugenzi Rasilimali watu huyo kuwa katibu.

Hivyo kanuni 4(3) isomeke kama ifuatavyo

**“kutakuwa na sekritariate itakayoundwa na maafisa kutoka Idara ya Rasilimali watu ambayo kiongozi wao atachaguliwa na Mkurugezi Rasilimali Watu kwa kushirikiana na Mkurugenzi Mkuu”.**

2. Kanuni ya 5(f) Kamati inashauri kuingizwa maneno **“kwa kuzingatia masharti ya sheria”** baina ya neno **“yoyote**” na “**itakayopangwa**”

Aidha, Kanuni ya 7 na 4 iangaliwe vizuri wajumbe watakaounda Kamati hizo kiuhalisia ziko kubwa pia zinalingana sana wajumbe wake.

Pia, suala la Katibu liwekwe katika utaratibu ambao tumeshashauri katika kanuni ya 4.

3. Kanuni ya 11(2) Kamati inashauri kufutwa maneno **“bila ya kuathiri”** na kuweka badala yaka maneno **“bila ya kujali”**
4. Kanuni ya 12 Kamati inashauri kuwekwa kwa proviso itakayosomeka kama ifuatavyo: **“katika utekelezaji wa ajira Bodi itapaswa kufuata masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni hizi”**
5. Kanuni ya 14 (3)(b)(d) Kamati inashauri watoke Wakurugezi wote na abaki Mkurugenzi wa Idara husika inayoguswa na uajiri wa mtendaji wake. Aidha, mtaalamu kutoka Ofisi Kuu ya Utumishi abaki kama mualikwa.
6. Pia katika Kanuni 14(7) Kamati ilitaka kufahamu ni nafasi gani Kamati ya Ajira itawajibika kwa Bodi ya wakurugenzi na zipi zitawajibika kwa Mkurugenzi Mkuu.

Kamati hivyo inashauri nafasi husika ziwekwe katika tafsiri.

7. Kanuni ya 16(a) Kamati inashauri kuandikwa vyema Kanuni hiyo kwani ikibaki hivyo si sahihi kwa kuwa imejumuisha jinai zote.
8. Kanuni ya 19, inarekebishwa kwa kuingiza maneno **“ya kuingilia kazini”** baina ya neno **“aridhilhali”** na **“iliyopo”**
9. Kanuni ya 22, Kamati inashauri kuzingatiwa utaratibu, wajibu na haki za mfanyakazi wakati wa muda wa majaribio ambao umeshakwisha ainishwa katika Sheria ya Utumishi na Kanuni zake.

10. Kanuni 24(5), Kamati inashauri kuangalia hali ya watu wenye mahitaji maalum katika kipindi hicho cha muda wa majaribio.

11. Kanuni ya 27(1), Kamati inashauri kuongezwa maneno **“kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma”.**

12. Kanuni ya 27(2) inarekebishwa kwa kufutwa maneno **“Na kukubaliana na mfanyakazi mwenyewe”** na kuweka badala yake maneno **“kulingana na utaratibu wa malipo kwa ngazi husika”.**

13. Kanuni ya 28(2), inarekebishwa kwa kufuta maneno **“kanuni hizi”** kuweka badala yake maneno **“Sheria na kanuni hizi na Sheria nyengine zinazohusika”**

14. Kanuni ya 28(3)(d), inarekebishwa kwa kufuta neno **“mwengine”** kuweka badala yake neno **“mengine”**

15. Kanuni ya 29 (2), haipo sahihi kwani sio jukumu lake kufanya marekebisho ikiwa madogo au makubwa yeye anatakiwa kupendekeza kwa Kamisheni ya Utumishi ambaye ndio yenye Mamlaka kisheria kuthibitisha Muundo na Mishahara ya Watumishi wa Umma kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma kifungu cha 25(0).

16. Kanuni ya 31, kuangaliwa tena mpangilio wa nambari za kanuni Ndogo hiyo kama ifuatavyo;

    (4) isomeke (3)

    (5) isomeke(4).

17. Kanuni ya 34(2), Kamati inataka kufahamu miongozo iliyotajwa katika kanuni hii inatokana na Sheria gani na kifungu Gani

18. Kanuni ya 42, imelekeza uzuri sana, Kamati inashauri Kanuni ya 29, iangalie utaratibu huu pia kwa masuala ya mshahara kama tulivyokwisha elezea.

19. Kanuni ya 50, Kamati inashauri kuangaliwa upya kwani ipo kiujumla iangalie kama ikiwa hakuna nyumba apewe fedha taslim kwa ajili ya makaazi.

20. Kanuni ya 53, Kanuni imeeleza uzuri lakini Kamati inashauri kuangaliwa tena Sheria ya Utumishi na Kanuni zake utaratibu ambao umeelezwa ili kuhakikisha kwamba haki inapatikana kwa mfanyakazi anayestaafishwa kwa namna hii.

21. Kanuni ya 54, Kamati inashauri kuzingatiwa Mamlaka ya Bodi, kwani yapo kisheria katika kuachishwa kazi mfanyakazi wa ajira ya muda.

22. Kanuni ya 119, Kamati inashauri kuangaliwa vyema kwa upande wa **kupokea zawadi** Kanuni hii ili kuepusha kuwepo kwa mgongano wa taratibu zilizokuwepo katika Kanuni ya Tume ya Maadili ya viongozi na kuchukuliwa hatua mfanyakazi huyo bila ya kosa kisheria.

23. Marekebisho ya Jaduweli katika Kanuni hizi ni kama yafuatayo:

    **a)** Kicha cha habari maneno **"upimaji wa kidaktari"** yasomeka "**upimaji wa afya"**

    **b)** Kicha cha habari maneno **"fomu ya kuombea nyongeza ya mwaka"** yasomeka "**fomu ya maombi ya nyongeza ya mwaka"**

Aidha, marekebisho hayo yaende sambamba na uandishi wa Kanuni husika.

Mbali na marekebisho hayo Kamati inashauri, Mamlaka ihakikishe kwamba inatoa uelewa kwa wafanyakazi juu ya haki, wajibu na fursa za watumishi ambazo zipo katika Kanuni hizi. Aidha, Kamati haikuona Kanuni inayompa fursa mfanyakazi kwenda masomoni kwa muda mrefu au mfupi ambapo kwa mujibu wa utaratibu wa utumishi mfanyakazi anaweza kuomba kwenda masomoni, ikiwa

ametimiza masharti ya ajira kwa mujibu Sheria ya Utumishi na Kanuni zake.

**Naomba kuwasilisha**

**……………………………………..**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**